# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, CHANGAMWE CONSTITUENCY HELD AT CHANGAMWE SOCIAL HALL

## ON

**3RD MAY 2002**

**CHANGAMWE CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, HELD AT CHANGAMWE SOCIAL HALL, ON 3RD MAY, 2002.**

**Present**

1. Com. Salome Muigai
2. Com. Paul Wambua
3. Com. Zablon Ayonga
4. Com. Prof. Okoth Ogendo

**Secretariat Staff**

1. Eunice Gichangi – Programme Officer
2. Phillip Mollo – Assistant Programme Officer
3. Regina Obara – Verbatim Recorder
4. Milka Mahindu – Sign Language Interpreter

The meeting was called to order by Sylvia Chidodo and started at 9.00 a.m.

**Sylvia Leli Chidodo:** Mabibi na Mabwana hamjambo? Karibuni sana hapa Changamwe, leo ni siku yetu ya pili kuwa nanyi katika Changamwe Constituency. Jana tulikuwa Mkindani Social Hall leo tuko hapa na ninawashukuru kwa kuja kwenyu. Ssasa kabla hatujaanza ningependa kwanza kuwajulisha kwamba commissionerCommissioners wetu ambao wako hapa leo., Jjana tulikuwa na wawili pekee, yake lakini leo tumebahatika tuko na wanne.

Kwanza kabisa nianze na commissionerCommissioner Salome Muigai ambaye tulikuwa naye jana, commissionerCommissioner Paul Wambua, CommissionerCommissioner Pastor Zablon Ayonga, na mwisho kabisa commissionerCommissioner Professor Okoth Ogendo.

Sasa kabla hatujaanza kikao chetu cha leo, tutaanza na dua alafuhalafu tutaendelea kwa hivyo twendelee.

**Dua:** Baba tunakuomba utubariki katika katibaKatiba yetu hii na utupatie msaada na utupe mapenzi yako kwani huu si ulizi ujuzi wetu, bali ni mapenzi kutoka kwako na tungekuomba ututie wema katika mazungumzo yetu; kila mtu ambaye atayeazungumza umpatie fahamu na aweze kuzungumza maneno yaliyo kweli na wale wanaosikiza vile vile, wawe ni wenye kuchukuwa maoni haya kwa uadilifu. ee bBaba tunakuomba utupe uangalifu zaidi mpaka tutakapo maliza kazi hii na utubarliki baba katika kazi yetu hii ili tuweze kufanikiwa kwa uongozi uwezo wako. Amen.

Na sasa nitunamkaribisha commissionerCommissioner Paul Wambua atuongoze katika hiki kikao chetu.

**Com. Wambua:** Salaam aleikum?. Sasa tutaanza kikao kupokea maoni yenu na kabla hatujaanza ningependa kuwauliza wale ambao wako na simu za mkono, - mobile phones, tafadhalini mzime maanake tunarecord proceedings na pengine zinaweza kulete hitilafu kwa kurecord. kKwa hivyo wale wana simu, tafadhalini zimeni. Nami naanza na kuzima yangu mkiona.

Basi yule atakaye kuwa wa kwanza kutoa maoni kulingana na orodha niliyopewa, ni Athman Mwasahani. Hilyo ndilo jina,? alafuHalafu, ni waeleze kidogo, ukija hapa mbele kama unatoa maoni bila kutupatia maandishi tutakupatia muda wa dakika kumi tu. Kama kuna memorandum ama maandishi utatupatia, tutakupatia dakika tano tu ueleze kwa kifupi yaliyoko kwa maandishi ama memorandum. Kwa hivyo wale ambao hawana maandishi ni dakika kumi, wale ambao watatupatia memorandum ni dakika tano tu umulike yale yaliyo muhimu alafuhalafu tuendelee maanake ninataka kila mtu apewe nafasi atoe maoni yake. Kwa hivyo tuanze na Athmani Mwasahani.

Kwa hivyo tuanze na Athmani Mwasahani.

**Athman:** Wakuu wa katibaKatiba, wazee, mabibi na mabwana salaam aleikum?. Mimi kwa majina naitwa Athman Mwasahani. Makao yangu ni Bomu c/o Mercy MasibilahiBilahi. Katika maoni yangu ambayo nimependelea kuyapeana, katika hii katibaKatiba ya Kenya, kuna serikali za mikoa ambazo tungependelea zifutiliwe mbali. Tunataka mfumo wa serikali ya majimbo, Ffederal government ambayo ndiyo itakayotuwezesha kutatua matatizo ya waKenyaWakenya. Kwa sababu, tuko na makabila tofauti tofauti na kati ya haya makabila tofauti tofauti kuna desturi mbali mbali ambazo kwamba kila watu wana mambo yao ambayo wanahitajikana kuyatumia. Na mengine yakitumika kwa wengine inakua ni hitilafu na hiyo huwa ni hatia.

Katika serikali, tunahitaji serikali kuu Kenya ambapo kwamba raisRais twataka achaguliwe kutokana kwa ma-gGovernor na at least apate asilimia thelathini kutokana kwa hawa magovernor ambao watakuwa wamechaguliwa na wananchi. Na katika kila jimbo kuwe na at least Mmjumbe mmoja kutoka kwa kila kabila ili aweze kuwakilisha watu wake. Katika hili jimbo kila jimbo inahitajikana liwe na bungeBunge, bungeBunge ambalo kwamba litaweza kusimamia mambo yake kupitia kwa Ggovernor. Huyu Ggovernor awe na mwanachini wake na msimamizi wa kifedha.

Upande wa elimu, serikali kuu ihakikishe kwamba kila raia amepata elimu ya kufaa. Upande wa usalama serikali kuu isimamie usalama wa raia; hivyo inamaanisha kwamba jeshi, maofficer wa upelelezi wawekwe chini ya serikali kuu. Afya,; serikali kuu pia iwe na uwezo wa kusimamia afya kwa kila jimbo.

Kati ya haya majimbo, kwa mfano kama Coast, mipaka ya majimbo kwa sasa ibakie kama ilivyo. Ila ila kwa majimbo mawili. hHayo ni North Eastern na Rift Valley. Haya majimbo mawili ikiwezekana yaweze kugwanywa kila jimbo mara mbili, hapo itaidadisha majimbo kuwa kumi. Kila jimbo liweze kuwa na bungeBunge lake ambalo kwamba litaweza kutatua matatizo tofauti, tofauti na desturi za watu.

Nikimaanisha desturi, hapa huwa mara nyingi tuna matatizo ya rasilimali za nchi. Hapo ni kitu kama mashamba. Wakati mwingine unakuta kunatokea tatizo baina ya, umejiwa na mgeni, unakaa na mgeni kwa muda pale anakuuliza, "bwana nimeishi na wewe hapa muda fulani kidogo lakini at least nipate mahali niweze kujisaidia hata nipate mboga kidogo". Na wewe unamwambia sawa ndugu yangu kwa vile tumeishi na wewe hakuna maneno, sehemu hii hapa unaweza kulima kujisaidia upate uwezo wa mboga;, lakini unakuja kustaajabu baada ya muda unakuja kuambiwa, " mzee ondoka hapa hili shamba sasa si lako ni la bwana Karanja" ambaye ulimkaribisha tu apate mahali padogo pa kuweza kujisaidia mboga. Lakini leo imekuwa wewe sasa uliyeokua mwenyeji kumkaribisha yule mgeni, unaambiwa hili shamba si lako imepatikana title deed hujui ile title deed pahali imepatikana. Unajaribu kwenda mbio kila unapokwenda mbio, kila unapokwenda hakuna mahali utasimama. Huna budi we ni mnyonge unafunga virago unaenda hapo umepoteza shamba lako lote ilai kwamba wewe ulizaliwa pale, babu , babu wa babu zako wote walitokana pale lakini leo, kwa ajili ya maandishi na ulaghai shamba lile umelipoteza. Kwa hivyo sisi waKenyaWakenya tuna hilo tatizo especially sana hapa Coast.

Mashamba mengi yamepotea na ndiyo hapa mpaka sasa hivi unasikia mara kwa mara kuna vita. Unasikia kesho, "oh kumetokea kumetokea huko kuna kayabombo". Kayabombo hii hujui pale imepatikana kumbe ni kwa ajili ya vitu, matatizo madogo madogo kama haya. Kwa hivyo ningependelea vitu kama hivi viweze kutatuliwa na wenyeji wenyewe. HaAlafu uuzaaji wa mashamba pia uwe na control. Wenyeji wawe wanahusishwa sio mtu mwenyewe binafsi, kuja kusimama na kusema "mimi nina shida hii na hii kwa hivyo shamba langu mimi nauliuza. AnNaliuza kiholela kwa bei duni- dhamani alafuhalafu baadaye unarudi unalia unaaza kulalamikia wenyeji,- wenzio "mimi nimenyang'anywa shamba, mimi nimenyang'anywa shamba" kianzilishi chake hakijielezi. Hhapo ndiyo kutakuwa na uwezo wa kuifanya nchi inasimama kikamilifu. Asanteni.

**Com. Wambua:** Asantei sana bwana Athman, ngojea kuna swali moja hapa.

**Com. Salome:** Asanti Asante sana bwana Athman kwa maoni yako. Mmimi nina swali moja. Uumesema kuwa tukishaa kuwa na serikali za majimbo kazi ya huduma za afya ya mwili itakuwa kwenye serikali kuu, masomo itakuwa kwenye serikali kuu, je nayo serikali ya majimbo itakuwa na kazi gani, unayo maoni gani juu ya ile kazi yenye tutaielekeza ile serikali ya majimbo

ama ile jimbo kule jimboni wakutakuwa wakifanya kazi zipi? Mgawanyo wa kazi za serikali kati ya serikali kuu na hii serikali ya jimbo?.

**Athman:** Nilimaanisha kwamba katika serikali za majimbo kuna kiwango ambacho tumeipangia kwamba serikali kuu itakuwa inapata 30%. Hii 30% itakuwa imetokana na serikali hii ya majimbo, ya jimbo fulani ambayo kuna kiwango chake cha asilimia sabini, hizo zinabakia kwa jimbo, asili mia thelathini zinaenda kwa serikali kuu. Hapo serikali kuu inakuwa ni kama taa kuangalia kama kuna mahali kumetokea hitilafu, hapo serikali kuu inaweza kuiuliza serikali ya jimbo, mbona hapa pamekuwa na hii pametokea hitilafu., Hhii hivyo inakaa kama ni jicho, na serikali ya jimbo ihuwezea kulitatua lile jaimbo kwa usawa.

**Com. Wambua:** Bwana Athman, nafikiria hakuna maswali mengine kwa hivyo tafadhali jiandikishe upande huu alafuhalafu tumpatie mwingine nafasi. T tutamuita Omar Mwinyi Shimbwa hilo ndilo jina? Okay Omar tafadhali.

**Omar:** Majina yangu kamili ni Omar Mwinyi Shimbwa mimi ni mwanaki mwananchti wa Changamwe, ni mwalimu kwa profession na kwa dakika hii ni mfanyi biashara. Niko hapa kutoa maoni yafuatayo kuhusu marekebishobadiliko ya katibaKatiba ambayo sisi hapa twashiriki zote. Kwanza kabisa msimamo wa serikali ambayo twaitazamia kutokamana na katibaKatiba mpya, ni mfumo wa majimbo, mfumo wa majimbo ambao kila jimbo litakuwa linajitawala administratively, politically and otherwise. Pia vile vile, mapato ya kila jimbo yawe yanasaidia jimbo lile na hasa upande wetu wa Pwani ambao umeachwa nyuma si kwa sababu katibaKatiba ilikuwa mbaya, ni kwa sababu tu ya uongozi mbaya uliokuwepo. Kkwa sababu katibaKatiba haikusema watu wa Pwani wanyanyaswe. K kwa hivyo tungeonelea katibaKatiba ambayo twaitunga hivi sasa, isisitize mfumo huo wa majimbo na sisi wenyewe tujitawale, tujitawale pia upande wa kiadministration, vile vile na upande wa kisiasa. Ttungependa sisi wenyewe kila mahali tulipo tuwe tunajitawala sisi ndiyo madiwani, sisi ndio Wwabunge na wale ambao ni wageni wawe wanatupigia sisi kura na sisi tuwe tunalinda haki zao, sisi tuwe tunawasimamia mambo yao, wao wawe wanafanya biashara zao, wafanye kazi zao na tuwe tunakaa kwa amani namna hio. Nna wale watu wetu waliopo sehemu zao waanafanye kama hivyo vile vile.

Twasema hayo kwa sababu kila mwananchi wa Kenya anatakiwa awe anajivunia matunda ya uhuru kufika miaka hii ya sasa. Leo tunapozungumza hapa kwa masikitiko ni kwamba, matunda hayo ya Kenya sisi hata hatuyajui, wacha kuwa tumeyaona. Ttumeelezewa katika kila vipawkao, katika serikali yetu ambayo ina Mmajeshi, ina polisiPolisi ina mambo ya Pprison , ina Mmauniversity, ina Mmacolleges yatoa mascholarships, ina Mma-pPermanent Ssecretaries, Mma-Aambassadors, Pparastatal Eexecutives na sisi katika hizo zote hatujakuwa represented kisawa sawa, hakuna quarter ambayo tumepewa!. Kila taifa jimbo liko represented katika vitu vyote ambavyo tumetaja hiviyo isipokuwa jimbo la Pwani pekee yake. Ukitafuta permanent secretary labda kama yuko utapata moja labda pekee yake, ukitafuta Jjudge utapata mmoja pekee yake kila unayetafuta. aAmbassador labda mmoja pia vile vile. Kwa hivyo tungependelea tuwe na serikali ambayo itakuwa na quotas katika mambo hayo,. kKukiwa na recruitment ya Aarmy ijulikane quoatao ya Pwani ni gani, ikiwa ni recruitment ya polisiPolisi, iwe hivyo hivyo vile vile na university za kitaifa iwe namna hiyo.

Kwa sababu tabia iliyoko hivi sasa yakija mambo ya kitaifa, mji wa Pwani huwa sisi hatuko, yakija mambo ya Pwani ambayo yaitwa ya kitaifa pia sisi vile vile hatuko. vile vile. Kama Ports yetu hii ndiyo rasilimali yetu kubwa, intaitwa ni national asset- sio asset ya jimbo ambayo yatakiwa iI-develop jimbo hii. Kwa hivyo itapokuwa inakuja upande wa mambo ya kazi na mambo kama yale, sisi huwa twaambiwa tukiweka watu wetu ni ukabila, watu wengine wakifanya huwa ni sawa sawa ni Kkikenya vile. Kwa hivyo twasema tuwe na serikali hiyo ambayo tumesema, ili tuweze na sisi kuona watu wetu katika kila nyanja katika jimbo letu hili. nNinapozungumza hivyo macommissionerCommissioner wetu hapa mtaniweia radhi, niko na hakika katika Ccommission yenu watu waPwani pengine percentage yao ni ndogo sana, si ajabu labda commissionerCommissioner ata hata ni mmoja ama wawili ; na wafanyi kazi wa Ccommission itakuwa ni hivyo hivyo pia vile vile. Kwa hivyo twaomba katibaKatiba itakayokuwa yaja, katika kila jambo la kiserikali, la kitaifa watu wawe wanapewa quota zao. Kila mmoja aone serikali hiylo ni serikali yake na aone watu wake wanamrepresent pale.

Vile vile katika serikali ambayo tuko nayo katika hii katibaKatiba serikali tuliyo nayo, inatulazimishia viongozi ambao hatuwapendi; namna gani? Kiongozi anashindwa kwenye siasa, kwenye kura halafu polisiPolisi wanatumiwa kuhakikisha kwamba kiongozi yule ashinde kwa lazima na tuna viongozi wengi amboyo ambayo wana mtindo kama huo. Na wanapewa madaraka makubwa katika serikali lakini badala ya kuwatumikia watu wao, huwenda wakatumia serikali kwasababukwasababu wanaona wamefanyiwa vyema favour na serikali. Hawawezi kutumikia watu wao, hawawezi kuwa sauti ya watu wao na wao watakiwa ndiyo wamechaguliwa ili wawe sauti ya watu wao. Kwa hivyo, katika katibaKatiba hii itakayokuja, tuhakikishe mambo kama hayo hayatatokea. Kura ikipigwa iwe atakayeshinda ndiye atakayekuwa mjumbe. Aliyeshindwa awe ameshindwa. Nazungumza kwa experience; 1992 nilishinda kura ya Mvita na nikapokonywa ushindi kwa sababu ya huu mfumo ambao tulionao sasa.

Pia vile vile katibaKatiba ya sasa haifuatwi. Hatuna protection katika huu mfumo tulionao sasa. Sheria ziko wazi kabisa. Hakuna "importation of voters" na watu wanafanya, lakini na kila mtu anajua. Unakuta sasa, tunapokuwa tunachagua viongozi wetu, hatuchagui kutokana na watu ambayo wako katika sehemu zile. Watu wanatolewa sehemu za mbali wanakuja hapa wanapiga kura na hawana haki zo zote katika area hii. Sasa sisi tumewachwa hapa kuwa twachaguliwa Wwabunge ambao sisi hatuwapendi, na madiwani ambao hatuwapendi lakini kwa sababu kuna mambo kama hayo, na serikali imefunga macho, haifuati katibaKatiba. Kwa hivyo hata katibaKatiba tunayoifanya sasa. ni lazima iwe itakuwa na protection. Isiwe ni katibaKatiba tutatunga, iwe nzuri lakini hakuna implementation. Lazima katibaKatiba hii ifuatwe to the letter.

Upande wa afya; tungependa serikali yetu kupitia serikali za mMajimbo pamoja na serikali kuu, kuwe na mfumo wa medical care ya wananchi wote kupitia NHIF. Contributions tunazo toa kwa NHIF, sziende kwa itazaidiana kusaidia watu kupata huduma bora za afya kwa sababu ni mfumo wa serikali kuwa kila mwananchi apate elimu, apate afya na vile vile awe ataondokewa na umaskini. Vile vile katibaKatiba hii tunataka kuomba ya kwamba, kuwe na diversification katika mambo ya kindustry. Hivi sisi kuna msongamano wa maindustries katika major towns. Tuzisambaze katika town zingine ili watu waache

kuhama makwao na kuja katika masehemu ya miji ambayo already yamejaa na services zimekuwa duni hivi sasa. Kuwe na distribution of industries katika miji yote ya Kenya ili watu waache ku-migrate na kusababisha mambo mengi ambayo yana adhiri miji mengine kwa namna mbali mbali.

Upande wa fisheries,- uvuvi, watu wa Pwani ni wavuvi na serikali yetu hii katika katibaKatiba yetu, hakuna namna yoyote ambayo imehakikisha wavuvi wamepata msaada. Kuna mambo ya deep-sea fishing, yameachiwa ma WaKorea waje wavue samaki wetu, wawamalize na sisi wenyewe hatufaidiki na mambo kama hayo. Tungeomba katika katibaKatiba mpya, serikali yetu itilie mkazo kuhakikisha wananchi wake wataweza ku-participate katika mambo ya deep-sea fishing na kuwasaidia wavuvi wadogowadogo katika mambo ya cold storage, e na mambo ya vifaa vya uvuvi na maswala mbali mbali ya mambo kama hayo. Kwa hivyo twaomba zile 100 nautical miles ziwe ni za wenyeji na the zile za second 100 nautical miles ziwe za watu ambao ni wa kutoka nje.

Mwisho kabisa upande wa elimu, tungependa somo la Rreligious education liwe compulsory kutoka primary mpaka level zote za elimu. Serikali ihakikishe kuwa walimu watapatikana na somo hili litafundishwa. Na katika hili jimbo tulilyosema, tungesema 60% ya rasilimali ziwe retained, 40% siende kwa serikali kuu ambayo itahudumia maswala ya internal security na mambo kama yale. Kwa hayo machache nafikiria nitakomea hapo na nitakaribisha maswali labda kutoka kwa commissionerCommissioner na wote ambao wamehudhuria katika kikao hiki.

**Com. Wambua:** Mimi ndiyo nitaanza lakini yangu sio swali, najua sheria iliyoko inasema kwamba 200 nautical miles ni za waKenyaWakenya hiyo ndiyo sheria. Kwa hivyo kama kuna watu wanavua kutoka nje, basi hiyo si halali. Kwa sababu najua hiyo ndiyo sheria ilioyoko sasa. Haijageuka.

**AthmanOmar**: Na sisi twaleta viboma hapa Likoni- walizama kituniwale samaki duni kabisa. Wale wazuri wanaenda nje.

**Com. Wambua**: Lakini hilyo ni jambo tunaschugulikia kwa ile task force nyingine. Kwa hivyo tutatatua huko. Sijui kama kuna maswali kwa bwana Omar. Haya basi jiandikishe pande hii alafuhalafu tumwite Ibrahim Musa Mohammed.

***E*brahimIbrahim:** Salamu aleikum wallahma tulahi wa barakatu.? Kwa jina naitwa Ibahim Musa Mohammed. Nafanya biashara ndogo ndogo hapa Mombasa. Kwanza kabisa ningelipenda kuzungumzia kwamba Kenya iwe tuwe na serikali ya majimbo. Sababu kubwa ya kusema hivyo, ni kwa kuwa nimeona kwamba serikali ya majimbo zitaweza ndio itaweza kutuhudumia sisi raia kwa urahisi na kwa ukamilifu.

Pili, nazungumzia kuhusu raisRais. Ningependekeza kusema ya kuwa kura ya raisRais ifanywe siku tofauti na zile kura nyingine ambazo tunapiga. Na kabla kura ya raisRais haijapigwakupigwa, napendekeza yule raisRais atakayekuwa anahitaji kura zetu, ataje majina ya mawaziri wake kabla ya uchaguzi haujafanywakufanywa. Hii itatusaidia kujua ni serikali ya aina gani raia

watakayokuwa nayo na itasaidia kujua ikiwa kuna waziri ye yote aliyetajwa pengine amewahi kufanya makosa makubwa watu ambayo ambayo watu wanaelewa, wanayaelewa kisha akachukuliwa tena akawekwa katika ile serikali. Kwa hivyo picha ya hiyo serikali tayari tutakuwa tumeiona kwamba kama ni ya majambazi, ama ni ya watu ambao tuna uhakika nayo yaani tuna imani nayo.

Kwa Mmawaziri; twapendekeza hawa Mmawaziri wasiwe Wwabunge kwa sababu mawaziri wakiwa Wwabunge, yule kiongozi hua anacheza nao kama kucheza zile button za tape recorder- anavyotaka anafanya kwa wakati wowote;, inaweza kuwa asubuhi, jioni akiamua anaamua tu. Lakini ikiwa ataanzia mwanzo itakuwa hapo kidogo tumemzuia hatakuwa hana uwezo wa kufanya anavyotaka mahali popote. Ningependekeza kwa uraia katika nchi hii ya Kenya, yaani makabila yaliyoko katika serikali ya Kenya yaandikishwe na mahali yaani province wanayotoka; kila kabila linakpo patikana. Viongozi wengine wote katika serikali napendekeza wawe ni watu wa eneo lile lile ambalo mtu anataka kulisimamia. Na raia wawe na uwezo wa kumkosoa raisRais iwapo atafanya makosa ya kumteua mkuu yeyote. Kkwa sababu utapata mtu anafanya makosa hapa kisha anachukuliwa mtu yule ananpelekekwa mahali pengine na kosa ni lilelile lingelikuwa ni mimi katika kampuni nimefutwa, basi recommendation recommendation zangu hazinikubalishi mahali pengine popote tena kuchukuliwa kwa kazi.

Katika katibaKatiba hii mpya, nilikuwa naiomba tume Tume iwapo kutatokea kifungu chochote cha katibaKatiba ambacho kitapingana na dini ya KuranQurani yaani kiislamKiislamu, basi kifungu kile cha katibaKatiba kisiwe kinamhusu Mmuislamu. Na upande wa stakabadhi za serikali kama vile kitambulisho, paspoti na makaratasi mengine yoyote ningependelea kuwe na katibaKatiba ambayo itatoa usawa katika tabaka zote za watu katika Kenya. Isiwe kwamba Mombasa tunaulizwa vitambulisho vya babu ambaye kwamba babu huyo mwenyewe wakati huo ilikuwa sio kenyaKenyaalipokuwepo, Kenya ilikuwa bado kuweko. Kenya ilianza kuwa wakati wa uhuru. Kwa hivyo atavyo atakalo ulizwa mtu Nyanza ama North Eastern, atakalo ulizwa mtu Nyanza , yaani vitu hivyo hivyo iuaulizwe mtu hapa Ccoast iwe vilevile kupata kitu hicho ambacho kwamba kitafaa. Na mimicoast. nNnilikuwanilikuwa napendekeza kuanzishwe home offices katika kila eneo, itakuwa rahisi zaidi kufanyia kazi hizo.

Kwa upande wa elimu,. Nnafikiri ndiylo kiungo kimoja muhimu sana. Na nNingependelea elimu zote zichukuliwe kama elimu kwa sababu elimu ni mtu kufundishwa apate kuelewa. Sasa ikiwa hii elimu hii yetu sisi ya dini ya KiislamKiislamu tutkitaaachiwa tu sisi wenyewe iwe haiko pale na sasa ma-time masehemu hayo ambayo twachukuliwa hawa wanafunzi wakasome, ndiyo sehemu time hiyo hiyo tena anatakikana aende akafanye tuition. Kwa hivyo ningependekeza elimu hii pia iwe absorbed katika sehemu system ile ile ya kiserikali na sio iwe IRE kama ilivyo syllabus. Iwe kama dini ya KuranQurani vile tulivyoilivyo kwa sababu ina tofauti kweli kweli kati ya hizi mbili. Tungependelea ichukuliwe kama ilivyo na serikali isimaie kama inavyo simaia hii elime elimu nyingine katika nchi. Ahsante.

**CommissionerCom. Wambua:** Asante sana Bbwana Ibrahim Musa nafikiria kuna swali moja hapa.

**Commissioner:Com. Ayonga:** Bbwana Ibrahim nataka unifanulie,

siku sikia vizuri, kama ungeweza kutoa nuru ulisema kifungo kifungu chochote kinachopinga kuranQurani . U ulisema hivyo? Umemaanisha nini? Siku elewa

**Ibrahim Musa:** Ssawa nilikuwa nafikiri ikiwa kuna swali linginenyingeni pengine ningeweza kuyajibu yote.

**Commissioner 1Com. Ayonga:** La, endelea na hilo alafuhalafu.

**Commissioner 2Com. Wambua:** Let us her ask the other questions then he can answer both.

**Commissioner 1:** Wacha aulize maswali swali la pilimawili alafuhalafu utajibu maswali yote mawili.

**Comm. Salome:** Asante sana bwana Ibrahim mimi nina maswali mawili kwako, ya kwanza ni juu ya mawaziri. , uUmesema mawaziri, aah presidentPresident mwenye angetaka tumchague atupe Mmawaziri wake baraza lake. Lakini umesema pia hao mawaziri wasiwe Wwabunge kwa hivyo sasa kuna uhusiano gani kati ya wananchi na Wwabunge, hao isipokuwa tu vile wamechaguliwa na yule raisRais sisi kama wananchi tuna uhusiano gani na hao Wwabunge hatujawachagua, si wanabunge kulingana na vile umesema.

Na pia nina swali juu ya hayo masomo ya kiislamKiislam ningetaka tafadhali unifafanulie vile ungetaka yahusishwe kwenye silabi ya masomo ya kawaida, asantei.

**Ibrahim:** Hili swali la kwanza la kifungu cha sheria ya kiislamKiislam katika dini ya kislam, katika dini ya Kiislam kuna u kuna vifungu vya sheria ambavyo kwamba vime elezwa wazi wazi kama kwa mfano urithi. Ssisi katika dini ya kiislamKiislamu tunarithishwa tukijua nitakupa tu example, kwa sababu mengine nikikuelezea si rahisi kufahamu. Ni kama vile Pprofessor amesoma miaka ishirini, alafuhalafu leo kwa dakika ishirini anielezee nifahamu- haiwezekani;, sasa na mimi nitajaribu kukuelezea kwa njia hio ili tufahamikiane. sSisi katika dini ya kiislamKiislamu, kama wewe ndio ndiwe ndugu yangu mkubwa na mimi ni ndugu yako mwingine wa kiume, tunapogawanyiwa urithi tutagawanyiwa sawa kwa sababu dini ya kiislamKiislamu imelenga ndugu wetu wa kike siku ye yote atakapoolewa si mashini ya kufetulia watoto tu ni mtu amekwenda na siku atakapokuwa kumetokea …………………. "Sitafahamu" yaani mambo yasiokuwa, yule atarudi, lakini katika ule urithi mimi na wewe tutapewa mwingi wa kuweza kumwangalia yeye, anauwezo wa kurudi pale na hatuna uwezo sisi wa kumfukuza mtu yule., moja.

Dini ya kiislamKiislamu imeturuhusu sisi kama waislamu ya kuwa tuoe wake wanne. Uutapata katika hizi hili sheria ambayo tunayzo aki-appeal haki ya pili akifanya chochote inaweza ikakumuhusu yeye kwamba yeye yuko right na ambapo hapo

atapingana na dini. Na sisi tunafahamu wazi ya kwamba hakuna mtu yeyote anaifahamu atakayekifahamu kitu chochote kuliko yule mwenyewe aliyekitengeneza kile kitu. Na na hakuna chochote kinachomfahamu mtu vizuri zaidi kuliko Mungu. kwa hivyo Aafadhali ni kukosee wewe lakini kuliko nisimkosee nimkosee Mungu. Nna hii ni sheria ambayo twaitunga kama sisi - , mimi ni Ibrahim Musa, siku moja utaniita "marehemu" lakini kuranQurani imetungwa na Mungu kwa hivyona hakuna siku tutamwita marehemu- bado atakuwa yuko pale pale.

Swali lingine nimeulizwa ni kuhusu mawaziri., Wwaziri sisi tunataka kiongozi anayetuwakilisha kule bungeBungeni lakini waziri hatuwakilishi, waziri ni mtu ambaye kwamba anaangalia - ni macho ya serikali kwa wizara fulani. Pengine, kwa hivi sasa nitasema naona ajabu nikisikia elimu Kenya ni sawa. M mimi nitasema elimu sio sawa kwa sababu tukifika hapa Mazeras tukianza kuingia ndani hutaamini kama ile ni Kenya na ni kilometre chache tu kutoka hapa. P pengine zile siku za nyuma siwezi kujua miaka, lakini kulinyesha mvua kukapita maji mengi mahali, Wwaziri akasema hapa patafaa mtambo wa kutolea umeme kwa haya maji yanayopita- alisahau ni kwa sababu ya mvua ya siku moja. tTukagharamia pesa nyingi …………… kutia -ni eneo lake hilo lile, tukatia ile na mahali pale hapana mahali ………… maligafi hakuna malighafi ya kufanyia kazi ile na ambapo pia kutoka yeye alipozaliwa alisikia kwamba Kkipevu kuna mtambo unatoa moto kwa miaka mia nyuma huko -bado inaendelea kutoa kutoa. lLakini pakawa hapafaitoi tena pale kwa sababu Kiswahili tunasema …………………….. "pashavusa limekuwa gogo halikuwa tena ……… bvoti". Kkwa hivyo tulichukua ule mtambo tukauweka, na baada ya siku chache unamkuta mtu anapita pale chini penye kina chajaa maji hapana chochote chochote; tunasubiri tena mvua ndio tutoe tena umeme. sSasa hii itasababisha yule waziri atakayechaguliwa atakuwa kuwa anafikiria jamhuri nmzima ya Kenya hata fikiria mahali pamoja.

Ni kama sasa hivi tunavyosema- samahani pengine nasema sana. Kuna mikoa fulani Kenya inayotoa mali nyingi sana ambazo kwamba, tunaweza kusafirisha kila mahali na kuna mikoa mingine inatoa kvitu ambavyo ambacho kwamba hakziwezi kujaza Ccharter moja -nazungumzia Ccharter ya watu sita sita, haiwezi kutoa. lLakini tukaweza kujenga uwanja mkubwa wa ndege pale tukawacha ile mikoa mingine. , kKwa hivyo hiyo itaweza kuzuia mtu kama yule asiweze kutufanyia, nafikiri ……………….. tumeelewana

Jambo lingine umeniuliza dini yetu ya kiislamKiislamu yaani tunataka ichukuliwe vipi katika IRE. , hHili neno IRE katika skuli, syllabus waliochukua wametuchukulia somo moja tu; yaani tume wame pin point some issues kutoka kwa ile dini ya kiislamKiislamu tukatia kwa ile IRE. lLakini katika kuranQurani kuna kuranQurani yenyewe, ni kitu mbali kuna hHadithi ni kitu mbali kuna ………….. "Ssaohidhi" ni kitu mbali, Kkunafiki ni kitu mbali, yaani kuna masomo mengi sana ambayo kwamba ukimuona mtoto wa kiislamKiislamu amesomea maneno hayo ni wewe pekee yako recommendation kablea sijakuuliza utaniambia "huyu mtu ana tabia nmzuri" kwa sababu amesoma ile dini ya kiislamKiislamu. Llakini ile IRE ni kiasi cha kupita ule mtihani tu na sidhani kama kuna mtu yeyote mwenye yani ameisoma asipewe karatasi. sSasa ikiwa atasoma IRE apate karatasi kwamba amefika amepita mtihani ule, kwa sisi waislamu tunahesabu bado hajasoma kwa sababu hawezi kuwa Chief Kadhi kwa chieve kazi kwa yale maswala yetu. Asante.

**CommissionerCom. Wambua:** Asante sana Ibrahim unaweza kujiandikisha pale alafuhalafu tutamuita Robert Kitunga.

**Robert Kitunga:** Salaam Aleikum.? Mimi majina yangu naitwa Robert Kitunga nimekuwa nikifanya kazi benki miaka mingi iliyopita kama ishirini, ishirini na mbili hivi. Na sasa ni mfanyi biashara. maoniMaoni yangu ni kama ifuatavyo,; viongozi wote, kuanzia kwenyu councilCouncillor, yaani Wmabunge na watu wengine lazima wawe na minimum qualification. Minimum qualification ya mtu kuingia katika kazi hio;, we cannot take every Tom, Dick and Harry kuchukua uongozi wa nchi hii. mMaanake nchi hii watu wengi wamesoma lakini unakuta katika mabaraza mengi- hata bungeBunge mtu education- standard zake ziko very doubtful. W watu wa ma EEEDED unawakuta hata katika Mmabaraza, hata katika bungeBunge. mMinimum qualification ywa mtu kuchukua uongozi Kenya iwe ni form four tena si form four, bure hivi hivi- uwe na minimum ya C grade ndiyo mtu anaingia kwenye uongozi uongozi; hatuwezi kuchukua mtu hivi hivi ati anaingia uongozi.

Ya pili, raisRais wa nchi hii apige vipindi viwili pekee yake; hakuna zaidi ya hapo. , aAkimaliza vipindi viwili akapumzike.

Ya tatu, hivi sasa unaona katika katibaKatiba hii ya Kenya, hakuna kifungu ambapo yule raisRais anamtaja running mate yaani yule Mmakamu wa raisRais. Makamu wa raisRais wa nchi anapaswa atajwe na raisRais na apigiwe kura na wanainchi sambamba na raisRais anavyopigiwa ili kwamba yule raisRais asiweze kumnyanyasa Mmakamu wa raisRais. Mmaanake hata sasa ukiangalia katika kifungu cha sasa somehow, sisemi wanichukulie vibaya hawale commissionerCommissioners. Inaonekana kama yule raisRais anamnyanyasa yule Mmakamu wa raisRais kwa kuwa hakuna kifungu kama hicho. Llakini ukiona katika nchi nyingi kama America, wapi, nchi zingine zilizoendelea utamkuta yule raisRais hawezi kumnyanyasa maanake yule Mmakamu wa raisRais pia amechaguliwa na watu kama yeye.

Tunakuja katika wale ambao ni mawaziri, watu wakubwa wa parastatals, majudge na nini. Wwanachaguliwa na raisRais na unakuta hawako vetted na Pparliament. Ssasa unakuta watu wezi, watu ambayo wanamakashiba wana makashifa ya wanawake, watu ambao wana tabia mbaya wanafanywa Mmawaziri. H hakika ni waziri gani anamakashiba ambaye ana makashifa tena mumfanye waziri, ni aibu. RaisRais anapochagua, yeye atakua na powers za kuwachagua wale mawaziri, lakini hawawezi kuingia katika ule uaziri mpaka wawe vetted na parliament. Il ili wale watu watakaokua vetted wawe ni watu wenye wauadilifu, wanyenyekevu, watu ambao wanapendeza kwenye jamii.

Hii habari ya presidentPresidential candidate kupata asili mia ishirini na tano katika kila Pprovince mimi mwenyewe binafsi sioni kama ili ni sawa sawa. Presidential candidate kwa maoni yangu mimi anapaswa kupata over 50% of the valid votes - zote katika nchi mzima. M maanake ikiwa raisRais, unaweza kusema tu anachukua 25%. Kkuna mikoa mingine mikoa midogo sana, anakwenda kuchukua support ya mikoa midogo mitano, ati anambiwa umepata 25%. Uukiangalia mikoa mikubwa karibu mitatu, minne hai-support yule raisRais na bado anaambiwa raisRais yshule aunaweza…………. *End of side A.*

***SIDE B***

***(Continuation)***

**Robert Kitunga:** …Hhakuna hata chama kimoja ambacho kinaweza kujivunia kinaweza kupata Wwabunge wengi ili kuweza kuunda serikali. Sasa pawe na provision ya government of national unity or coalitioncollision ambapo yule mkubwa wa kile chama chochote chenye Wwabunge wengi, anaweza kuunda coalition na vyama vingine na pengine tunaweza kusema yule mkubwa wa kile chama, aweze kuwa prime ministerPrime Minister nabasi auunde serikali. Maanake labda pengine hakuna chama chochote ambacho kina uwezoa wa kuunda serikali kwa kuwa labda hakikupata Wwabunge wengi. H hili swala la raisRais kwamba ati anakuwa above the law, ni raisRais gani wa dunia anaweza kuwa above the law? Ikiwa Clinton kunshika kumshika tu matiti Lewinsky au kumhadaa yule Lewinsky, anafikishwa mahakamani, kwa nini raisRais wa Kenya hawezi kufikishwa mahakamani wakati anapokuwa kwenye ofisi?. H hilo ni jambo la kutatanisha maanake raisRais ni binadamu, anaweza kufanya makosa, he can be corrupt, anaweza kufanya economic crimes, kwa nini yule raisRais anaambiwa hawezi kushtakiwa while in office?., Mme, I don’t believe in that. Mmaoni yangu ni kwamba raisRais yeyote wa nchi hii atakayeshika madaraka akipatikana na makosa, ashtakiwe while in office kama vile alivyofanywa Clinton.

Tunakuja kwenye mambo ya corruption;, nchi hii imejaa corruption. Nnafikiri kama sikosei, labda ni namba tatu namba nne kwenye dunia nzima - ttunazungumza dunia nzima. Ttunakwenda wapi? Where are we heading to? Na hii nchi ni tajiri; lakini sasa kuweza ku-checkuchange corruption kuwekwe sheria ngumu, security punitive measures ku-curb corruption. Hhata ikiwezekana wajua hata ikiwezekana , - mimi sizungumzi katika hizi sheria za sharia ,- lakini mimi ni nasema ikiwa kama sisi tulikuwa tunachukua a hundred people ambao wamefanya economic crimes na ambao wameiba mabillion ya nchi hii, tuwapeleke stadium wafanyiwe firing squad unafikiri kuna watu wengine wa nyuma wanaweza kufanya corruption? Nani atakayefanya corruption ikiwa tunaona watu wanapigwa marisasi?, Iikiwa watu wanapigwa risasi stadium na mtu aliyoko nyuma anajuwa mimi nikifanya corruption nitapigwa risasi, hii nchi ingekuwa ni nchi maridhawa, safi tena.

Tunakwenda kwenye uchaguzi wa mamayorMamayor;, mamayorMamayor, Mmachairmen wa Llocal Ccounty councilCouncils na nyingine. Nni aibu kwamba ati Mmacouncillors wana…

**Com. Wambuamissioner:** Robert uko na dakika mbili, tafadhali umalize.

**Robert:** Haya; Kkuna Macouncillors thelathini na sita kama hapa Mombasa, wanachagua councilMaylor mmoja; na huu mji una watu zaidi ya millioni moja unusu, millioni mbili, hii sheria ianze tena sasa, kwamba mamayorMamayor wote wa Ccity

councilCouncils, wa Llocal councilCouncils wachaguliwe directly na by the people na tena ikiwezekana ifanywe siku maalum ambapo wale mamayorMamayor pamoja wa Ccity councilCouncil, wa Mmunicipals wa na Llocal councilCouncils watachaguliwa siku maalum sio kwenye elections, hiyo itakuja baadaye.

Na kuna hili swala la watu kama hapa, kama Coast hili iko sana., Uunakuta mtu amejenga nyumba yake katika kiwanja cha mtu, surely amekaa kwa miaka thelathini, miaka arobaini amelipa rates miaka yote hiyo lakini bado anaambiwa wewe ni kama squatter. Jjamani kwa nini isiwekwe sheria kwamba mtu akikaa ijapo ijapohapo miaka mitano tu, wewe una haki uzungumze na yule mwenye kiwanja akunuzienulie ile title deed ili na wewe pia uwe na kitu cha kujivunia; wewe walipa kodi tu, rent miaka arobaini wewe mwenye kiwanja anakuambia 'wewe lipa tu' ukija ukipiga hesabu ya ile rent uliolipa ya tosha hata kulipa kile kiwanja mara mbili au mara tatu., Nndugu zangu, hayo ndiyo maoni yangu. Kama kuna commissionerCommissioners wowote wanaotaka kunihoji, naomba mimi nakaribisha maswalioni yao.

**Com. Wambuamissioner:** Asante sana Robert. Uulitaja kuwa presidentPresident awe na two terms pekee yake lakini hukusema kipindi kiwe cha miaka mingapi.

**Robert:** Kipindi ni kama kawaida - miaka mitano mitano. Aakitoka hapo aende nyumbani akapumzike.

**Com. Wambuamissioner:** Haya ngojea nafikiria kuna swali kutoka ...

**CommissionerRobert:** Kuna swali nyingine kutoka kwa commissionerCommissioner.

**Speaker from the audience:** You were very clear.

**CommissionerRobert:** I was very clear?.

**Com. Wambuamissioner:** Haya mzee unataka kuuliza swali? Lakini utaipitisha hapa kwa huyu mwenye kiti - halafu.

**RobertSpeaker from audience:** Mimi nina swali lingine wacha nije huko jukwani.

**Com. Wambuamissioner:** Keti, keti, keti., Robert, ukizungumza upitie kwenye kwa mwenye kiti tafadhali.

**Speaker:** Bwana Robert amezungumzia qualification za candidate wanaogombea uchaguzi tu lakini hakutuambia qualification za mayorMayor au za presidentPresident wanatakikana wawe na qualification gani. Nna swala lake neno lake la mwisho kuhusu wale renters wa plot hii, yule huwa si squatterkwota huwa ni renter. Kkwa hivyo hata katika nyumba, waweza kukaa miaka mia lakini hujakuwa na uwezo wa kuinunua ile nyumba unayokaa. Asante.

**Com. Wambuamissioner:** Maswali ni mawili Bwana Robert ufafanue tu.

**Robert:** Nnitafafanua., Unajua mayorMayor wa mji, nafikiri ata hata Uhuru Kenyatta alizungumza habari yake., mayorMayor wa mji ikiwa qualification yake at least ni form four yenye C grade yule mayorMayor lazima awe highly qualified, mtu ambaye amefanya kazi isiopungua labda miaka kumi kwenye good private institution, ambaye pengine anajua mambo mengi, he is transparent mambo ya accountancy na nini, ili kuwa akiwa held Hhead kwa ile Ccity councilCouncil ………… watu wake wengi watamfuata kwa ule uadilifu wake-, experience matters. Yyou cannot just take anybody just because he is a form four umfanye mayorMayor., Ile maanake kuna lazima at least awe ten years experienced katika private sector amehojiwarudiwa amekuwa Mmanager, amekuwa Aaccountant, amekuwa nani, ili kusudi ata hata barua zake zinaonyesha akipewa mayorumayor ata-run mambo yaende shwari. Swali lingine lilikuwa nini -, la hawa watu wenye nyumba. Hhawa watu wenye nyumba, hawa watu wenye nyumba mimi according to me, kweli kama mtu amekaa miaka thelathini, arobaini, kwa nini wewe mwenye kiwanja usifanyea mpango kumuuzia yule mwenye plot au mwenye ile nyumba ili awe yeye mwenyewe pia ana ploti?. K kwa maoni yangu mimi ni wewe umuuzie maanake ni kama unamnyanyasa.

**Com. Wambuamissioner:** Asante sana Bwana Robert jiandikishe upande ulehio. Tuna ndugu na dada zetu ambao hawaelewi ile lugha ya kawaida ambayo tunaongea na tuko na mtafsiri. Kkwa hivyo ataangalia kama wako hapa na kama wako atajaribu kutafsiri yale ambayo tunayasema hapa. Sasaalafu tutamwita Stanbuli Nassir, kabla hatujamwita mama mmoja mwingine alafuhalafu azungumze. Kkwa hivyo Stanbuli. Tulimpatia nafasi,- tulisikia maoni yako huko Mvita? ya Llakini sasa wewe usirudie yale uliosema. Kkama kunauko na mapya sasa utuambie yale mapya, yale ulioyasema bado tuko nayo yako kwa record.

**Stanbuli:** Kwanza kabisa napenda kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kunipa furrsa hii tena kuongea hapa, nawashukuru Mma- commissionercommissioner, wazee wangu na ndugu zangu mliowalioketi hapa kunisikiliza. Kwa jina mimi najulikana kwa jina lya Stanbuli Abdulahi Nassir. M mimi kwa hakika kwa ufupi nia manalharakati; Ssihusiki nkwa chama chochote cha kisiasa lakini zaidi naingilia harakati hiyno kutokana na uzoefu niliyo nao na makaratasi ambayo yanashughulikia sana haki za watu wa Pwani, ambao miaka sitini na mbili walikuwa wakiwakilishwa Lancaster Hhouse na wajumbe wawili ambao mmoja wao ni mzazi baba yangu mimi mzazi. K kwa sababu ya kuwa mtoto wake wa kwanza, zile karatasi niko nazo mimi na kama mabwana Mmacommissionercommissioner walinilivyoeleza nimewai kuongea chandaria Chandaria lakini niliongea mambo fulani na leo nitaongea kuhusu mambo mengine alafuhalafu, pengine tukikutana pale Baluchi, nitamalizia kwa sababu kwa muda munaotupa wa dakika tano au kumi, hatuwezi kuzungumza yote ambayo yanahusu wenyeji halisi wa sehemu hii ambao kwa ujumla ni Waswahili.

N na hili liko wazi kama sehemu mliokpo hapa, ni watu wa Changamwe na hili ni kabila moja katika Wwaswahili. Kkama tunavyoelewa, tunaingilia upande wa ardhi. Wwa cChangamwe wana ardhi zao na kwa kulingana na mkataba niliokuwa

nimewapa, sehemu ya tano inazungumzia kuwa kuna watu walio na free hold titles ambao walikuwa hawapaswi kulipa kodi. Nndugu Robert hapa aliyetoka amezungumzia mambo ya masquatter. Z zaidi, mkataba huo kama tulivyoelezana ni kuwa haukutekelezwa. Kkwa hivyo wachangamwe Wachangamwe wengi wametupa ardhi zao na mpaka leo wanadhulumiwa na hawawezi kujitetea mahali popote - ndiyo tunakuja kama sisi tunaoelewa kuwaeleza ninyinyinyi. Huu upande wa ardhi ni muhimu sana Mmacommissionercommissioner muutilie mkazo kama tulivyokuwa tunaongea sitaendelea zaidi ya hapo. Llakini katika pia kuangalia mambo ya ardhi, ni muhimu sana mujue wachangamwe Wachangamwe ni nani? Si anayeishi tu changamwe Changamwe. Wwachangamwe kuna mbari tano; kuna mbari ya Mmwenye Kkitue, kuna mbari ya Mmwenye Mmgosi, kuna mbari ya Mmwenye Mmfaki, kuna mbari ya Mmwenye Kkoba, kuna mbari ya Mmwenye Nngovo.

Sasa tukija upande wa elimu, Kenya ni nchi moja ambayo ime-saigni mkataba wa declaration ya United Nations 1948 Uuniversal Ddeclaration for of Hhuman Rrights. Na kwenye chapter tano ya paragraph sabini na nanetano chapter hiyo inaeleza kuwa hakuna mtu yeyote atakayezuiwa ku-enjoy uhuru wake wa dhamiri- freedom of conscience, freedom of thought, of religion, freedom to change his religion or belief and freedom to manifest and propagate his religion or belief in worship, teaching, practice and observance. Kifungu muhimu ndugu ma-commissionerCommissioner ni hichi kinachosema “every religious community shall be entitled at its own expense, to establish and maintain places of education and no such community shall be prevented from providing religious instructions for persons of that community. No person attending any place of education shall be required to receive religious instructions or to take part in, or attend in any religious ceremony or observance; and no person shall be compelled to take any oath whichoath, which is contrary to his religion or belief”.

Sasa tukija kwenye katikati ya hichi kifungu kwa “kilacha any religious community itaruhusiwa kubuni, kujenga na kuendeleza mfumo wa elimu wanaotaka wao,” . K kkabla ya uhuru ndugu commissionerCommissioners nyote, na pengine ndugu Wambua zaidi kama ulivyokuwa umeeleza chandaria Chandaria uliwai kusoma shimo la tewaShimo la Tewa Tewa kama sikukosea;, sasa shimo la tewaShimo la Tewa ni moja, kuna ambayo inaitwa Serani, zamani ilikuwa ikiitwa Arabph Bboys, kuna Mubaraki ambayo sasa ni Araph Arab Girls kuna Miyome ambayo sasa hivi inaitwa Mombasa Polytechnic. Kwa iInitials za Miyome ni Mombasa Institute of Muslim Education. Kuna Nahamisi Secondary school, hizi shule zote kabla ya Kenya kupata uhuru ni shule za wenyeji wa sehemu hii ambao ni wafuasi wa dini ya KiIislamu., Llakini baada ya kupata uhuru hizi shule tulipokonywa na serikali na wakazichukua na wakazipeleka watakavyo wao, na wakafanya watakavyo wao. S sasa hivi shule inayoitwa Mombasa Institute of Muslim Education ambayo ni Mombasa Polytechnic si ya Wwaislamu tena na asili mia inayotakikana ya Wwaislamu wasome pale, hakuna tena. Kwa sababu hii, katika katibaKatiba mpya ambayo mtatunga tunataka mtusisitizie tafadhalini kwamba, institutes - tasisi zote ambazo kabla ya uhuru zilikuwa ni za wenyeji wa sehemu hii Wwaisalamu, warudishiwe wenyewe na misaada kama ile inayopewa mission schools na serikali na shule hizi na taasisi hizi zipewe bila ubaguzi wowote. Hilno ni upande wa mashule.

Kuna na mtindo au mfumo ambao unaotumika sasa hivi wa kuwa walimu wanahusika na somo la dini ya Kikristo. Kkwa sababu kuna Cchurch na Sstate zinashirikiana walimu wengi wanaweza kwenda university na wakawa wanasomeshwa

kwaenye expense yza serikali wanazochangiwa na church.  L lakini hatuoni university vijana wowote Wwa Kislamu ambao wanalipiwa na Sserikali na Mmisikiti au Iinstitute za Kkislamu ambao wanasimamiwa kusomeshwa elimu ya dini ya Iislamu. Ttunaomba pia hii mulitilie maanani ili liweze kutekelezwa kama ipasavyo.

Sasa tunawacha upande wa elimu tunakuja upande wa uchumi.  Miradi mingi ya uchumi ambayo imefanyika katika mkoa wa Pwani tangu uhuru mpaka hivi leo, mengi imezoroteka na mengine imeya kufa, na hakuna dalili yoyote ya kuonyesha kama serikali, au wanaojaribu kudai wanatuwakilisha, kuwa wanakwenda mbio na kujaribu kuyafufua miradi hiyo kwenye mkoa wa Pwani.  Kkama ni kuhusu pesa katika bilioni mia mbili na tisa ya pato la serikali, bilion hamsini inatoka Pwani.  Inasiksitisha sana wakati kama sisi tunajua hata kuna millionaires hamsini humu humu ambao ni wenyeji, ambao kila mmoja wakati hana pesa ni milioni mia tano, mambo haya yote yamepuuzwa na sisi tunajua ni njama ambayo inajaribu kuweka watu wa Pwani wawe nyuma - na njama hiyo haikuaanzwa na serikali -, serikali wameridhi tu; tuelewane vizuri.  Nnjama hiyo ilinaanza na Mmuingereza na Mmuarabu kabla.  K, kwa sababu nikisema kwa nini naifuata  tume Tume kila mahali nitoe kidogo kidogo, nafikiri tulizungumza na nikasema niko na ushahidi mwingi ambao sitaweza kuutoa mara moja.

1914 mpaka 1918, kuna Rregistrar wa land ambaye anaitwa Dolasi.  Wwakati wa Mmuingereza sehemu ya Sabaki, Malindi palikuwa pakiitwa Paliani.  Aameeleza kwa kirefu ambapo nitakupatia ushaidi wakati wa Baluchi hall, kuwa watawala ambao walikuwa ni maliwali hapa, Saralee- bin- Salem na Seik- bin- Sala kwa niaba ya Ssultan na ma-Ggovernor waliokuwa wakitawala hapa, walichomea watu majumba na wakawafukuza alafuhalafu wao wakarudi wakayanunua.  N na mambo kama haya yametokea sana kwenye mkoa wa Pwani ndio tukawaambia mtie maanani kwa sababu, kutoka uhuru wamepuuza wanaosimamia utawala sehemu hii; either kwa kuwa hawataki au wanachagua nani wanamtaka wanamendeleza.  Ssasa tukija kwenye swala la *(Interruption by the commissionerCommissioner).*

**Com.  Wambuamissioner:** Tafadhali Stanbuli dakika ni mbili tu, malizia- malizia tafadhali.

**Stanbuli:** Sawa;, Kkuna tatizo la utawala sasa upande waa polisiPolisi.  Ddakika hii nikiongea na nyinyi, sehemu fulani za Mombasa polisiPolisi wanaanza kazi saa mbili usiku tayari hata kama unatoka msikitini, unaweza kushikwa. Llakini inasiksitisha kuwa kwenye miji yetu kwa kulingana na sheria ya Kenya, ya policePolice law, hairuhusiwi ukahaba wa wanawake wala wanaume.  Llakini ukahaba unaendelea na ikibidi, hata nyinyi ma-commissionerCommissioner mkitembea usiku kwa makini unaweza kukuta sehemu polisiPolisi amekaa na kahaba mahali pamoja.  Tunataka mtilie mkazo jambo hili tusichukuliwe kama endangered species - sisi pia ni binadamu nai tuna misingi yetu ya kimaisha ambayo tungependa ilindwe.  Kwa kwa hivyo misako, kama ni kuja kufanywa misako iwe itaanza baada ya saa fulani kama ilivyokuwa zamani;, sio mapema wakati hata sisi wengine hatujatoka kwenye misikiti - na hata ukitoa kitambulisho, inakuwa afadhali siku hizi Kenya ukutane na mwizi kuliko kukutana na polisiPolisi,.  Ssababu hatabado ukitoa kitambulisho bado utakwenda.

Kwa hivyo tafadhalini katika kupanga katibaKatiba zenyu za sheria za polisiPolisi, mturekebishie tusichukuliwe kama second-

class or third- class citizens inchini Kenya wakati kwa historia na sheria, hakuna Mmkenya mwingine yeyote aisipokuwa sisi, watu wa Pwani, aliyekuweko kabla yetu sisi. ,S sisi tuko hapa zaidi ya miaka elfu mbili kama yuko ambaye amefikisha muda huo ajitokeze mimi niko tayari. Kwa hayo machache nawashukuru kwa kunipa fursa hiilo sina la zaidi, isipokuwa naomba Mwenyezi Mungu atupe fikira njema na busara tuweze kumaliza mambo haya kwa makini kama itakikanavyo. Asanteni sana.

**Com. Wambuamissioner:** Swali moja Bwana Stanbuli.

**Comm. Salome:** Asante sana tena kwa maoni yako, mimi nina swali moja. Uumesema habari ya ukahaba hukubalishwi na katibaKatiba iliyoko sasa kwa wanaume ama wanawake. katibaKatiba tuliyoko nayo sasa wakati huu, inaweka uzito mkubwa sana kwa ukahaba wa wanawake; Jje wewe umesema haukubalishwi kwa wanaume ama wanawake; ungetaka kuona mambo gani yakifanywa ili ikatazwe kwa wote wanaume na wanawake usawa?.

**RobertStannbuli:** Kwa hakika nilichosema ni kuwa kulingana na Kenya policePolice law, ukahaba hauruhusiwi nchini Kenya. N na kwa kama ingekuwa muda munawezaniruhusu, niko na ushahidi wa kuwa under section mia moja na hamsini na tatu mpaka section mia moja hamsini na sita ya Kenya policePolice law, ukahaba ni kitu ambacho hakifai na hata nyumba za kukodisha ili kuenda na angalau kahaba, kama mtu ana ushaidi wa jambo kama hilo ni kushtaki au kueleza polisiPolisi na inawachukuelia hatua. L lakini jambo hili tumeliona ni la mazoevu tu kwa tulivyonauzoevu wa kuwa hii ni sehemu ya ma-tourists sana - tunaona ukahaba ni kitu cha wazi ni kama ni sheria inalilinda. Ttunaloomba ni kuwa sheria hiylo litekelezwe kama ipasavyo, isipuuzwe. Hhatujasema kuwa hakuna; iko sheria lakini haitekelezwi na ndio nikatoa mfano kuwa unaweza kutembea town, unakuta askari amekaa na kahaba wanaongea kama ni mairungilundi wanakula pamoja, kama ni sigara pamoja na ukipita kwa mbali anakuiitae na anakushikae na yeye amekaa na huyo hapo. Nafikiri nimejibu sawa sawa.

**Com. Wambuamissioner:** Asante sana Stanbuli tafadhali jiandikishe pande hii. Tutamuita mama atupatie maoni ya akina mama, tutamuita mmoja Riziki Muthokaola.

**Riziki Muthokala:** Mabibi na mabwana salama aleikum?. Mimi kwa majina naitwa Riziki Muthoka nimekuja hapa kwa niaba ya Upendo Women’s Group. Nataka kutoa maoni yangu na. hasa nataka kugusia kwa upande wa waujane. K kwa mfano, kuna pengine msichana na mvulana wamependana pengine wenyewe wameona, na msichana ana kazi na mvulana pia ana kazi. W wenyewe wametafuta mali yao, wamejiendeleza, wameezaa watoto wao, kwa bahati mbaya mume anakuja pengine anakufa ghafla. Ssasa hapa utaona wale mashemeji wanaanza kumnyanyasa yule mjane. P pengine ameachiwa mali yake, wale mashemeji wanataka kumpokonya ile mali yake. Kkama ni shamba wanaingilia kwa upande wa mashamba wanataka kumpokonya ile shamba ili pengine waliuze na yule mjane yuko pale pale na watoto. Kkwa upande huo naona wajane wananyanyaswa sana.

Jambo lingine ni kuhusu upande wa mahospitali., Hhospitali zetu za sasa twaona sisi tunanyanyaswa. Ppengine mama ameenda

pale hana chochote na ni mgonjwa. Uukifika pale ile kadi pekee yake, unaambiwa utoe shilingi thelathini ndio umuone daktari; zile shilingi thelathini huzipati, wewe mwenyewe huna chochote ata hata utakuta yule mama amelala pale au yule mzee ameketi pale nje, ameambiwa "toka nje" na yeye zile shilingi thelathini hazipati hazipati. Ssasa hapo pia ningependelea pengine serikali iingilie kwa upande huo.

Jambo lingine ambalo ningetaka kuliongea ni kuhusu ardhi. H hili jambo la ardhi limeturudisha nyuma sana. K kwa mfano, babu yangu amekaa hapo, babangu amezaliwa hapo, mimi mwenyewe nimezaliwa hapo, alafuhalafu sasa baada ya kuwa wale wazazi pengine wamefariki, baadaye unakuja unaambiwa wewe uko squatterkwota na hujui kwenyu ni wapi. Uumezaliwa pale pale, umelelewa pale pale hujui kwenyu ni wapi - unajua kwenyu ni pale alafuhalafu baadaye unakuja unaambiwa uko squatterkwota hujui uende wapi. H hilo pia ni jambo lingine ambalo naona ninaambiwa linatunyanyasa sana.

Jambo lingine ambalo ningependa kuligusia ni uaajiri wa kazi; sisi wanawake tunanyanyaswa sana. Tukienda kwa kampuni labda unatafuta kazi, yule boss ama yule tajiri pale, unahitaji kazi anakwambia "lete kitu kidogo". Na kitu kidogo kile, si kuanzia pengine shilingi mia; anataka kama shilingi mia tano kuendelea. Aama akuambie "njoo ofisini" sasa unashindwa, kule ofisini unaenda nini! Kkesho ukirudi ukienda ofisini anakuanzmbia mambo mengine ama anakuambia anataka mapenzi na wewe ndio anikuajiri kazi. S sasa hapo naona sisi wanawake tunaona tunanyanyaswa ki- upande huo sana. Maoni yangu ni hayo, Asante. Mwenye swali ajaribu kuniuliza.

**Com. Wambuamissioner:** Asante sana mama, jiandikishe upande huo. kidogo. Wacha tusikiza tusikize mama mwingine mmoja Rukia Hassan.

**Rukia Hassan:** Asalama Aleikum kwa nyinyi nyote mlioko hapa?. Mimi kwa majina naitwa Rukia Hassan na niko hapa kwa niaba ya akina mama wenzangu ambayo tuko Changamwe, nikiwa kama kiongozi wa Women Development, Changamwe Division. Ya kwanza, nazungumzia kuhusu uongozi - awe ni councilCouncillor, awe ni Mmjumbe. LaNni kwanza lazima huyu Mmjumbe au councilCouncillor awe kwanza, sharti la kwanza, awe ameoa aikiwa ni mwanaume na ikiwa ni mwanamke awe ameolewa. Na na pili achunguzwe mienendo yzake kabla haja ruhusiwa kusimama mahali popote. Kwa sababu ni makosa - nikisema hivyo kwamba hivyo ni kwa sababu ni makosa huwa yanatutokelea sisi akina mama, taabu nyingi twazipata sisi, twaambiwa tuchague mCcouncillor au mbungeMbunge kumbe watu hawa si watu watu wa maana, sio watu wadilifu ni watu wa kutupeleka huku na huku, - hawawezi kutusikiliza sisi na hatuwezi kuwaambia mambo yetu ili waweze kututekelezea. Kkwa sababu tukichagua councilCouncillor tunamchagua kwa niaba ya sisi wananchi, lakini anapokwenda katika councilCouncil yeye hafanyi kulingana na vile tunavyotaka. Kwa hivyo ni lazima achunguzwe kwanza akiwa ni councilCouncillor; kwanza awe ameoa, pili kama ni mke awe ameolewa, alafuhalafu pia achungunzwe nyendo zake akiwa ni mwizi au yoyote vile, asiweze kuruhusiwa kuchaguliwa.n Hhiyo ni ya kwanza.

Ya pili, wanawake wanaiomba serikali ya Kenya, wapewe kitu kiti kimoja kila wilaya katika nchi nzima ya Kenya ili waweze

kuwakilishwa vizuri kule bungeBungeni. Nni jambo la masikitisho kwamba Kenya hii nzima na bungeBunge lake lote lina wanawake sita pekee yake ambao wamechaguliwa!. Kkwa hivyo tunaona kwamba sisi wanawake hatuwakilishwi kule katika bungeBunge inavyopaswa kwa sababu wakilishi wetu ni wachache. Kukitolewa Bbill ya kuhusu mwanamke, haitekelezwi maanake kura ikipigwa zitatoka kura sita pekee yake. Nyingi zitakuwa za wanaume tutakuwa hatukuwakilishwa. Kkwa hivyo tutaomba kila wilaya kutoke kitu kiti kimoja kipiganiwe na wanawake pekee yake bila kuingiliwa na mtu yoyote - wilaya hizo zote za nchi nzima nafikiri wanawake watawakilisha kikamilifu kule., Hhiyo ilikuwa ni ya pili.

Ya tatu -, mtanisamehe kidogo wajua sijazoea kuongea sana kupendeza mbelre za watu lakini nitajaribu. Tunaomba pia serikali iweze kuweka makao ya watoto ambayo wazazi wao hawawezi kuwalea watoto wao vizuri, au wameshindwa na nguvu za kuwalea na pia kusaidia wale wasichana wanaopata mimba nje ya ndoa - kuwatupa wale watoto. Kkwa sababu kukiwa na makao kama hayo wewe ukimpata mtoto ametupwa mahali hutaogopa kumchukua, utamchukua umpeleke pale au mzazi akijua kwamba hawezi kumtunza mtoto wake kwa njia ipasavyo, au kumpa elimu inayotosha atampeleka pale kwa kwenye yaile makao ili aweze kuangaliwa, serikali ichukue lile jukumu la kumsaidia. Kkwa kusema kweli umaskini nchini umekuwa mwingi zaidi. k Kiasi kwamba utamuona mtu ameng’ara akiwa nje lakini hajiwezi kwa mambo mengi. Kwa sababu uchumi umekuwa chini, kila kitu kimekuwa sasa hakina bei - tuseme hakina dhamani. Kama ni biashara ukifanya ni nyingi katika sehemu hizo, ni hiyo hiyo unakuta mapato yanakuwa kidogo. Kwanza ilikuwa twapata mapato kupitia vibanda na nini na nini, lakini vibanda vilipofunjwa sasa ndiyo umasikini umezidi zaidi. Hilo pia sio sababu kubwa ya kwamba umasikini umeletwa kwa sababu ya ufunjaji wa vibanda, la!, Yyaani wizi wa Ccorruptioon umekuwa mwingi katika Kenya. Aliye juu hamwangalii yule aliye chini. Anataka kupanda juu zaidi badili ya kuschuka chini kumwangalia aliye chini. Kwa hivyo tungeomba serikali ijaribu kutufanyia hayo makao. Yatapunguza pia utoaji wa mimba na pia akina mama kuwatupa watoto hovyo.

Ni jambo la kusikitishka kama juzi hapa Changamwe pia, kuliokotwa mtoto katika hii hii ward ambayo tunakaa leo. Mtoto mzuri, mwenye afya nzuri lakini masikini akawa amepoteza maisha yake. Ametupwa na mama akawa amepotea ameingia mijini, hajulikani ako wapi. Kama makao yangekuako hapa karibu nadhani huyo mtoto hangetupwa. Angepelekwa pale katika mwenyewe angeendakua anasemea “mimi siwezi, ni nazaa lakini huyu mtoto wangu namweka hapa”. Ingekuwa pia ni rahisi. Kwa hivyo kwa kuszaidia vkitu kama hivyo tunaomba serikali ituwekee makao kama hayo kila sehemu ili tusipoteze hawa viongozi ambayo wanatupwa na kuwangamizwa. Ppengine kesho wangekuwa ni viwaongozi wazuri - kama tunavyosema katibaKatiba aibandilishwe. Hata katibaKatiba ikibandilishwa, ikiwa kiongozi atakangeyekwenda pale hatakuwa kiongozi mzuri, basi katibaKatiba itakuwa vile vile - haitafuatiliwa.

Kwa hivyo ni sisi mtujaribiye kutuwekea makao kama hayo, pengine tunaowazaa, tunaogopa kuwalisha tukiwapeleka pale badalaili ya kuwAyonga watakuwa ni viongozi wazuri baadaye.

La mwisho ni kuhusu habari ya ardhi. Kupitia kwa akina mama wanaomba kwamba akina mama wamekuwa sana hawapati urithi katika ardhi. Na pia utakuta mama amenjenga pengine nyumba yake mahali katika plot ya mtu. Amekaa pale na mwenye

plot kila mwezi anamdai pegine mia tatu, mia nne. Ikiwa ndani ya mwaka moja hajalripa, utakuta mwenye kiwanja anachukua jukumu la kumpeleka yule mama kortini., Hatimaye nyumba yake inauzwa kwa sababu ya kukosa kulipa pesa za kiwanja. Kwa hivyo tungeomba pia serikali ichukulie zile ploti ambazo ni za serikali wamepewa wenye viwanja wanasitumikia, wazsinunue ili waweze kutuszaidia sisi ambayo tuko katika zile ardhi. Tunanyanyaszwa tukilipa kodi kila mwezi, kila mwezi na ukishindwa kulipa hatimaye nyumba yako inapotea na pengine una watoto, wale watoto wanaanza kuhangaika huko na kule na wanakosza mahali pa kukaa.

Na la mwisho kabisa, nilikuwa nimesahau;, Kkatika huu upigajie wa kura, uandikishajie wa kura, I mean; tunaona makosa yanafanyika katika sehemu zetu. Kama ni sheria, ma- commissionerCommissioner tungeomba mtwambie kama ni sheria; Kkwa sababu utakuta mtu amesimama Changamwe na anakwenda, pengine yeye amekuja hapa sio Mchangamwe yuatoka pengine nje ya Changamwe, badailai ya kutafuta wana- Changamwe ndiyo wamjue kama yeye ni mzuri, ataenda kwao kama ni Kitui, Nairobi, sijui wapi, anaenda kuwandikisha kule kura alafuhalafu wanakuja kupigia hapa. Jameni amri hiyo iko? Kwa sababu unakuta wakati wa kura tunategemea kuwa tunaenda kumshinda yule mtu ambaye hatumtaki amesimama, yeye ndiyeo atepayevuka mshindi kwa sababu kura simetoka kwao. Tunaomba kama hiyo amri mko nayo tunaomba mwifute kwa sababu watu wa Pwani tunanyanyasika kwa sababu hiyo. Tunashindwa kuwachagua watu wetu tunaowapenda kwa sababu kura zimendikishwa mbali zinaletwa hapa. Siku sikifika za kura unaona mabogi yanaschuka, yakischuka ya naschuka na kura za Changamwe. Kwa kweli hilo jambo linatuumiza sana. Kwa hayo mafupi mimi nasema ni asante, ndiyo maoni yangu.

**Com.missioner: Wambua:** Mama ulisema kiongozi yeyote akiwa councilCouncillor ama MP awe ameoa?. Je akichaguliwa na apate talaka, aondoke kwa madaraka ama unasema je?

**Rukia:** A-aham kwa sababu ile, tayari tuliona kwamba alikuwa ameolewa na tabia nzuri., Llakini sasa wajua makosa ndani ya nyumba hutokea saa yingine wanaume hawapendi sisi akina mama - akiwa ni mama ,- hawapendi kumuona mama akischugulika juu ya mambo kama haya., Bbaba atakubali mama achaguliwe, akisha chaguliwa muda kidogo utamuona kwa vileakikwambia una husiana pengine na ma-commissionerCommissioner khukaa pamoja ana aunza wivu wivu na kusema "wewe sikutaki tena". Huyu hatumchukulii kama – huyo ametalikiwa., Llakini yule ambaye anataka kuchaguliwa sasa, awe ameoa na awe ameolewa na pia na kiwango zcha elimu kiwe zcha juu kwa sababu kukosa elimu ndiyo tunakuwa pia tunapeleka uongozi vimbaya.

**Com. Wambua:** Swali ingine kutoka kwa Ccommisisoner.

**Com. Ayonga:** Mama Rukia, umesema kwamba wanawake wapewe kiti kimoja kila wilaya?. Sijui kama ulifikiria kama tuna wilaya ngapi Kenya, kwa mana tuna wilaya kama sabini na nne. Yaani hiyo nikusema wanawake sabini na wanne wapewe viti vya bure. Kabla hujaendelea mbelre, nataka pia nikukumbushe kwamba katika wingi- population ya Kenya, wanawake ni wengi sana. Wanawake wako asilimia hamsini na mbili (52%) Wao ni wengi sana kuliko wanaume. Mbona wanawake wangeipenda wapewe na wakiiwa wao ndiyo wengi? Lazima kuna mambo fulani fulani ambayo si sawa, kwa maana watu

mkiwa wengi mtafanya mpendavyo?

**Com. Wambua**: Ngoja swali la pili mama.

**Rukia**: Hilo ni la pili, sio?

**Com. Wambua**: Si utajibu pamoja?

**Rukia:** Nitajibu pamoja kama amenipita, mtanisamehe maanake huoii umri wangu ni mwingi.

Lile swali bwana commissionerCommissioner la kusema kwa nini akina mama wanataka mwapatiwe viti vya bure, ni wazsi na ni kweli, kwa sababu akina baba mumetuongoza miaka mingi mpaka manyumbani bado mnatuongoza. Kkwa hivyo ata hata tukiwa bungeBunge tumekuwa wengi, pia hakuna wasi wasi tunaweza tu kuongoza bungeBunge. Tukipewa nafasi.

**Com. Salome:** Mimi nina swali kwako mama. Nina maswali mawili, moja ni nikukukumbusha swali moja ulilouliizwa ni kuwa akina mama tuko wengi kwa nini hatuchaguwi akina mama wenzetu. Kwa hivyo ni kukukumbusha tu usikilie utanijibu. Langu la kwako ni lile la kusema ni lazima kiongozi awe ameoa ama ameolewa. Tuna watu wengine viongozi wetu wa dini kama ile ya katoleki, hawaoi wala hawaolewi. Je kutitokea mmoja hapa, kama askofu ama Bpabpa parokio akataka kugombea kiti za ujumbe, kuwa mbungeMbunge ama kuwa diwani nayo hayo tutafanya nini nayo.

**Rukia:** Huyo bwana unasema akiwa ni papaBaba au akiwa ni kasisi, tayari ana cheo kanisani. Kwa hivyo akichanganya huko itakuwa anataka kuchanganya mambo mengi. Kwa hivyo tunayemtaka ni yule niliyemasema mimi;, ni mtu tu wa kawaida - awe ni muumini wa kanisa au ni muumini wa msikiti, ushzasikia?. Ikiwa yeye ni kasisi au ni kadhzi hatuwezi tena kumchagua kwa sababu ana wadhifa mwingine tayari anaushikilia dani ya dini. Kwa hivyo watu ni wengi, kule kugawanyana makazi lazima tuwachiane nafasi kwa wengine.

Na lile la pili la kuhusu wanawake ni wengi, kwa nini hatuwezi kuchagua. Tunaweza lakini huwa hamtupi nafasi. Kwa mfano mama akiingia hapa sasa hivi, asimamea anawaotaka ubunge katika Changamwe hii, tayari tuna mbungeMbunge ambaye ni mhesimiwa wetu. Bbasi kutafanyika mbinu za hali ya juu ili kusudi sisi akina mama tumchukie ma mwenzetu tu simchague. Kwa hivyo ndiyo sababu tunaomba vile viti vyetu ambavyo yule mbungeMbunge atakeyekuako tutamchagua, na yule mama pia tumchague. Ndiyo sababu nikaomba hivyo. Asante.

**Com. Wambua:** Asante sana mama. Kwa hivyo jiandikishe hapa. Hilyo swali ambalyo unataka kuuliza hiyo ni kazi yetu kama commissionerCommissioners. Formulas sisi ndiyo tutatengeneza. k Kwa hivyo sio ya mama. Asante sana.
Sasa tumwite Mugandi Mulai.

Sasa tumwite Mugandi Mulai:

**Mugandi**: Salam aleikum. Mimi kwa majina ni Mugandi Mulai Mugandi na pia ni chaiman wa Kanu Miritini Ward. Nimekuja hapa kutoa maoni yangu kwa tume hii ya leo ili tujenge Kenya yetu kwa miaka inayokuja.

Mimi kwa maoni yangu nasema serikali ya wilaya ifutwe na tuweke serikali ya majimbo. Na maana ya kusema hiyo sio kusema at jimbo fulani……………. *continues to tape 2*

# Tape 2

**Com. Salome:** Wengi hatuchagui akina mama wenzetu, kwa hivyo nakukumbusha tu ushikilie tu, utanijibu. Swali langu kwako ni lile la kusema ni lazima kiongozi awe ameoa ama ameolewa. Tuna watu wengine viongozi wetu wa dini kama ile ya Katoliki pahali watu hawaoi wala hawaolewi. Je kukitokea moja hapa kama askofu ama Baba Paroko akataka kugombea kiti cha ujumbe kuwa mbunge ama kuwa diwani, naye hayo tutafanya nini?

**Rukia:** Asante Madam. Huyo bwana unayesema akiwa ni Papa au Kasisi, tayari yeye ana cheo kanisani kwa hivyo akichanganya huko itakuwa anataka kuchanganya mambo mengi. Kwa hivyo tunayemtaka ni yule ndiyo nasema mimi ni mtu tu wa kawaida. Awe ni muumini wa kanisa au ni muumini wa msikiti. Wasikia? Lakini akiwa yeye ni Kasisi au ana kazi, hatuwezi tena kumchagua kwa sababu ana wadhifa mwingine ambao tayari anaushikilia ndani ya dini. Kwa hivyo watu ni wengi kule kugawanya makazi lazima tuachiane nafasi kwa wengine.

Na lile la pili kuhusu wanawake ni wengi kwanini hatuwezi kuchagua? Tunaweza lakini huwa hamtupatii nafasi. Kwa mfano mama akiingia hapa sasa hivi asimame anataka ubunge kwa Changamwe hii, tayari tuna mbunge ambaye mheshimiwa wetu. Basi kutafanyika mbinu za hali ya juu ili kusudi sisi, akina mama tumchukie mama mwenzetu tusimchague. Kwa hivyo hiyo ndiyo sababu tunaomba vile viti vyetu ambavyo yule mbunge atakayekuako tutamchagua na yule mama pia tumchague. Hiyo ndiyo sababu nikaomba hivyo. Asante.

**Com. Wambua:** Asante sana mama. Kwa hivyo jindikishe hapo. Hilo swali ambayo unataka kuuliza ni kazi yetu kama Commissioners. Formulae ndiyo sisi tutatengeneza kwa hivyo sio ya mama. Asante sana.

Sasa tumwite Mugandi Mulai.

**Mugandi Mulai:** Salamu aleikum?. Kwa majina ni Mugandi Mulai Mulandi na pia ni Chairman wa Kanu Miritini Ward. Nimekuja hapa kutoa maoni yangu kwa tume Tume hii ya leo ili tujenge Kenya yetu kwa miaka inayokuja. Mimi kwa maoni

yangu nasema, serikali ya wilaya ifutwe na tuweke serikali ya majimbo. Na maana ya kusema hivyo, sio kusema ati nimesema kuwe jimbo fulani , - nimeona hivyo kwa sababu viongozi wale wa Serikali yaitakayokuwa ya majimbo wanaweza kukaa katika jimbo lao na kupitisha mambo yao kwa kulingana na maendeleo ya kimaisha. Maisha ya maendeleo; kuna majimbo fulani katika Kenya ambayo yamewachwa sana nyuma kimaendeleo,; kwa barabara na hii ni kwa sababu katika serikali kuu, huwa kuna majimbo fulani hayana uongozi mzuri. Nasema hivyo kwa sababu, viongozi wale waliyochaguliwa kule mbele pengine labda huitwa waoga ama huwa pengine hawasemi, lakini wana uwezo wa kusema lakini baadaye huwa wanapingwa.

Kitu ambacho ningependa kuiomba serikali na pia tume Tume hii ya KatibaKatiba inayoendelea ni kwanza, serikali ya majimbo iweze kuwaunga wale viongozi watachaguliwa wakae katika wilaya yao / jimbo lao, waweze kupitisha mambo yao, wapange ile rasilmali ambayo wanapata katika jimbo lile. 70% waweze kutumia katika jimbo lile and 30% ya ile iende kwa serikali kuu. Na serikali kuu ikiwa imepeleka hizo vitu, wajumbe wa jimbo lile lingine wawe wanaweza kuasilisha kule kwa serikali kuu ili kusudi kuwe na uwezekano wa kugawanya maendeleo katika nchi.

Kwanza nikisema kama mkoa wa Pwani, mimi nikiwa kijana wa mkoa wa Pwani, hapa Changamwe nimezaliwa hapa, kuna matatizo mengi ambayo yako na wananchi wengi wadogo wanapata taabu hasa kuhusu ardhi. Wamenyanyaswa, ardhi hawana na viongozi ama wale wenye uwezo huja wakayanyakua iyale maardhi wakishirikiana na viongozi ambao wako serikalini kama machief na maD.O. Wananchi wanapata taabu sana. Haya ni maoni yangu na maoni haya nayasema kwa Kamati hii, iweze kuchukuliwa muhimu kwa sababu sasa watu wa Pwani tumekuwa na taabu ya kutosha.

Tukienda kama njia hii ya kwenda Kaloleni, mwisho wa lami ni Kaloleni;, huko mbele hakuna lami na huko mbele, kuna watu ambao wana biashara ambao wanakuja town lakini wakati wa mvua hawawezi kuja town. Tukienda njia hii kwenda Kwale, unapata mwisho wa lami ni Kwale. Kwenda Kinango na sehemu nyingine kule hakuna barabara. Njia ya Dandini, hakuna barabara. Ndio sababu nasema uongozi si mzuri sana katika serikali. Na nikisema hivyo ni kwa sababu nimetembea Kenya ijapokuwa si kutembea sana, nimeenda sehemu zingine za nje nimeona barabara hadi porini na hazina kazi lakini lami iko na hakuna chochote kinachotoka huko. Kwa hivyo maoni yangu sio mengi nilikuwa nikitaka kueleza hayo kwa machache ili kuona kwamba hayo niliyoyasema yametekelezwa. Ahsanteni.

**Com. Wambua:** Asante sana Mugandi. Kuna swali? Jiandikishe upande huu. Halafu tutamuita Gideon Mutemi.

**Gideon Mutemi:** Kwa majina naitwa Gideon Mutemi Maluki. Mimi naishi hapa Changamwe. Jambo la kwanza ningependa kulizungumzia ni kuhusu nomination ya members of parliament. Mambo ya kunominate MPsS inasitahili kutupiliwa mbali. Maanake hatutaki selected MPsS. Tunataka elected MPsS.

Jambo la pili, ningependa kugusia kuhusu kutoa cheque ambazo ni bogus. Bogus cheques kulingana na sheria za sasa sio crime. Kwa hivyo ukimdai mtu, atakuepuka kwa kukandikia cheki ambayo haina pesa kusudi mwachane. Kisha ukimfuata sana,

atakwambia nenda kortini. Ukienda kortini, kuna process ndefu sana. Naona hakika kwa wanyonge, inaumiza wananchi wa kawaida.

Jambo la tatu ni kuhusu sheria ya receiver ship: Eemployers wengi wanatumia hiyo sheria ya receivership kunyanyasa wafanyikazi. Maanake kwa hakika kampuni nyingi sio kufilisika zinafilisika lakini ni namna ya kutafuta jinsi watakavyo umiza wale wafanyikazi. Hhuenda ikawa tajiri ana kampuni zaidi ya moja, kisha atauzhamisha assets za kampuni moja kwa kampuni nyingine, kisha atafute court orders kuonyeshana kuwa amefilisika na hali hajafilisika.
CommissionerCommissioners, ningepeana mfano? Naruhusiwa?

**Com. Wambua:** We zungumza yale unayoyataka kuzungumzia na uhakikishe hutapitisha muda ambao tunakupatia.

**Mutemi:** Kampuni ya Kenya Bus Mombasa, kampuni iliyoandika cheques za milioni saba ambazo zilikuwa hazina chochote. Wafanyikazi hao wamekuwa kwa shida, kupata haki yao ni shida na hakika ningeomba serikali ichunguze zaidi kuhusu cheki hizo. Ahsante

**Com. Wambua:** Okay Bwana Mutemi asante sana. Unaweza kujiandikisha upande huuii. Sasa tunamwita Mjaa.

**Mjaa:** Mimi majina yangu ni Mjaa Jumba, mimi ni mzaliwa wa hapa Changamwe. Mapendekezo yangu mimi napendekeza majimbo. Na ukitaja majimbo, mnaona watu masikio yawainaruka. Kama watu wa bara wanaona kama watafukuzwa, sijui watafanywa aje? Majimbo si hivyo;, majimbo ni kushirikiana. Tunataka majimbo ili kujilinda na haya makabila makubwa. Huwa kila kitu cha vamia Ppwani. Kwa usemi utaambiwa Kenya moja lakini kwa ukweli ni Ppwani moja. Hakuna mtu wa Ppwani aliye na robo acre bara isipokuwa hapa karibu, kwanzia Lunga Lunga mpaka Lamu, hizi ardhi zote ni za watu wa bara. Sijui ni kwa sababu za kupewa 'mlandi' au wenyewe waliuza, lakini mtu akicheza vizuri bara, huko ndiko atatuzwa ardhi, lakinikama hapa hata ucheze vipi, hupati kitu kule?

Kitu cha pili nazumgumzia mahakama ya kadhzi. Kadhzi ipate korti nkidogo na korti kubwa. Isiweo kama hivi sasa. Case yaweza, kusemwa katika korticase ya kiislamu kisha wakati wa pili ikaenda korti ambayo si ya kiislamu. Kwa hivyo korti ya kiislamu iwe Llower court na Hhigh court. Mtu akishindwa katika korti ndogo anaweza kupata rufani aende katika korti kuu. Itakapo kwisha hukumu hapo, iwe hapo ndipo mwisho isiende katika korti hiyo nyingine.

Jambo la tatu ni kuwaama uwezo wa raisRais usiwe above the law, uwe chini ya sheria. Kwa hivyo tunawalaumu Wwabunge wetu wengi kwa kuwa hawatufanyii kitu na nini, lakini kwa unguvmu wa raisRais ulioko, mbungeMbunge huogopa kusema kitu. Imefikia hata raisRais aseme jambo la muhali kwa mfano kama aseme kaa ni jeupe, basi wajumbe wote huchangia , hawajaona kitu cheupe kama kaa. Kumpeleleza kumbe sio ujinga ama nini, ni hofu, leo huungi mkono utakuwa hupati uwaziri, na leo ukiwa waziri basi utatolewa uwaziri. Kwa hivyo tunaona wajumbe wetu wako weak kumbe ni uoga; , lazima kukisemwa kitu ukiunge

mkono ili mambo yako yaende vizuri.

Kwa upande mwingine, yasikitisha kusikia mtu akisema kuna chungwa lakini hakuna mchungwa. Nikisema hivyo, ni kama kusema, kuna Kiswahili lakini hakuna Mmswahili. . Sijui mMtu huyo akipelekwa kama Port Reitz akienda akipimwa huwa ana akili au sijui atasemaje daktari. Useme kuna Kkikamba lakini hakuna Mmkamba, au kuna Kkiingereza lakini hakuna Wwaingereza. Kwa hivyo ninaiomba serikali neno kama hili waliondoe. Waswahili ni taifa kama vile bwana mmoja alitaja mengi, lakini yote yatangazwea ni Wwaswahili. Na niakisema Wwaswahili tuna hata Wwahindi ata hata Wwajaluo. Kkila kabila waliozaliwa hapa, yeye anaweza kusema ni mMhindi lakini ukimwamkua kKihindi hajui, au asema ni mMwarabu ukimwamkua kKiarabu hajui. Huyu mtu huwa upande wa wWaswahili. Kwa hivyo naomba hilo jambo serikali ilitilie mkazo sana. Kwa sababu ni muhali kusema kuna chungwa lakini wasema hakuna mchungwa.

**Com. Wambua:** Ni hayo tu?. Basi...

**Mjaa:** La mwisho lategemea hizi ardhi. Inakua watu wa hapa wanakuwa victims. Mtu kwao anasema ni hapa lakini anajenga nyumba anatozwa kodi. - m Maneno kama haya natilia mkazo maana yashasemwa. WMalipao, wmalipao maisha sijui mpaka lini. Serikali sijui yapendelea au vipi? Hapa kuna ardhi za Mombasa walitoa amri watu wanunue mashamba, wanunue zile ploti za majumbe lakini ajabu hukuo kwetu serikali imenyamaza tu, haijasema chochote. Kwa hivyo tungeliomba pia kwa mfano kama mtu ameishi miaka thelathini na bado analipa, amelipa pengine hata ile bei anayonunulia shamba ashaipita,; hatusemi wanyanganywe lakini ifanywe tasimini mtu anunue. i Ile hali leo iwe naye akiwa njema kwani uanaweza kwenda benki, upate mkopo. Jambo kama hilo serikali yataka iangalie sana.

**Com. Wambua:** Asante sana Mjaa. Nafikiria hatuna swali kwako kwa hivyo ujiandikishe kwa hiyo meza. Halafu tutamwita Jack Okwirie.

**Jack Okwirie:** Asante sana ma-commissionerCommissioner na wananchi wetu watukufu wa Changamwe. Kama mlivyosikia, jina langu ni Jack Okwirie, na mimi sana sana nashugulika na kuwahamsisha wananchi juu ya ulemevu - yaani mimi ni mwenye kiti wa D.A.R.T. ambayo inamanisha Disability Awareness RaisRaising Team. Na hapo pia nimekuwa mwenye kiti wa Ford Kenya, Port Reitz Ward, nimekua mwenye kiti wa NDP, Port Reitz ward mpaka hivi sasa vile mnavyiojua mambo yamekuwa. Kwa hivyo, katika mazungumzo yangu nitazungumzia mchanganyiko wa mambo ya disability na mambo ya siasa pia. Kwa hivyo kwanza kabisa, ninaomba kuwe na sheria kwamba sign language iweko katika television na wakati wote kunakuwa na mkutano wa hadhara ili kusaidia wenzetu ambao ni walemavu ambayona hawezi kusikia yale ambayo yanaendelea.

Jambo la pili, ninaomba walemavu wapate representation katika quaroteras zote. Naomba katika councilCouncil wakati wa uteuzi wa macouncillors tuwe na representation ya kiasi fulani kama 10% ili hawa walemavu waweze kuwatetea walemavu katika councilCouncil kwa sababu, inaonekana wale ambao wanaingia hasa wananchi wetu ambayo wamejaliwa, wako sawa

sawa, wako na kiburi, wako na kiburi sana ya kuwanyanyasa walemavu. Unakuta councilCouncillors wanapewa nafasi katika maunisicipaa na councilCouncillor huyu ana walemavu katika eneo lake na hatoi nafasi kwa mlemavu. Kwa hivyo tunataka walemavu wawe represented katika councilCouncil. Katika bungeBunge tunataka representation pia, iwe katika Cconstitution. Kati ya wale ambao wanateuliwa na raisRais, tuwe na walemavu wa kuangalia haki ya walemavu katika bungeBunge.

Jambo lingine, katika makampuni kuwe na sheria kwamba kila mwaka kampuni inapoajiri wafanyi kazi, kuwe na 10% imeteuliwa kwa walemavu ili walemavu waondoke katika hili jangwa la kutokuwa na kazi. Kuna kazi nyingi sana ambazo zinaweza kufanywa na walemavu na unakuta wanapuuzwa. Unakuta mlemavu ana elimu ya kisawasawa lakini kwa sababu ya kiburi cha yule aliyeko katika Mmanagement anaona mlemavu kama mtu asiye kuwa na maana. Kwa hivyo, hapo naomba iwe hivyo. Naomba pia katika katibaKatiba kuwe na free education kwa walemavu. Kwa sababu hayaii mambo ya walemavu yaimefanya watu wengi sana wazazi wengi, wanaficha hata watoto walemavu manyumbani; na kuwe na sheria ya kuwashtaki wazazi ambao wanaweka ama kuficha watoto walemavu. Tunataka watoto wote walemavu waende shule, wapelekwe katika vituo ambavyo wanaweza kurekebishwa ili waweze kujisaidia wao wenyewe.

Pia naomba katika Cconsititution yetu, bad languages ya kuita walemavu, unasikia mtu anaita mlemavu "kiguru, kiwete, kipofu, kiziwi" - lugha hiyo iwe prohibited katika Cconstitution. Iwe ni sheria kwamba unapomwita mlemavu kwna lugha hiyo ushtakiwe. Kwa sababu hiyo lugha inamaanisha mtu asiye na uhai. Ki-Vi class katika Kiswahili inamanisha kitu ambachzo hakina uhai. Kwa hivyo wakati unapomwita mlemavu lugha hiyo, unamaanisha unamrudisha chini kabisa katika hali yeye hana uhai. Na sidhani kama kunma Mmlemavu yeyote ambayo amelemaa kiasi ambacho hana jina. Kwa hivyo lugha hiyo tunataka iondoke kati yetu.

Naomba pia tuwe na sheria ,- nakumbuka kuna wakati raisRais Moi alichangischa zaidi ya milioni ishirini na mbili na mimi ndiyeo nilikuwa mwenye kiti katika Mombasa District ya kupendekeza jinsi pesa hizi zinaweza kusaidia walemavu. Na tangu hapo nafikiri ni kama miaka ishirini na miwili iliopita, hakuna faida yeyote ambayo walemavu wamepata mpaka sasa. Nafikiri riba ambayo imepatikana hapo inatosha kuwasaidia walemavu wale ambao hawajapata kazi. Na iwe ni jukumu la serikali kuwapatia walemavu kazi na yule ambaye hajapata kazi, awe anapata kiwango fulani cha kujisaidia.

Nikiingilia upande wa siasa, ninaomba hivi;, Kkatika katibaKatiba cheo cha raisRais iwe inazunguka kwa mikoa. Kwa mfano, hivi sasa Mkoa wa Central Province tumeshapata kiongozi kutoka Central Province na sasa tumeshapata kiongozi kutoka Rift Valley. Ssasa tumebaki na Province sita, - Nyanza, Western, Nairobi Province, - na ninaposema Nairobi Province sio kwamba kuna kabila fulani wamevamia hiyo province tuseme ni wao ndio wenye hiyo nchi. h Hiyo province ya Nairobi ni province ya Wamaasai. Kwa hivyo ninaposema Nairobi province ninamaanisha Wamaasai,. Eastern province, Ccoast province na North Eastern Province. Ni provinces sita. Kwa hivyo katika katibaKatiba tuwe na katibaKatiba ambaypo itnafanya sasa hizyo mikoa sita ndiyo wanatoa wale ambao wanagombea uUraisrais. At least province moja itatoa raisRais, ili sasa Uuraisrais uwe unazunguka katika provinces. Hii ndiyo itasaidia nchi yetu kwa sababu nchi yetu imepagawa na ukabila na kuna makabila

mengine ambayo, they pretend that they are more equal than other tribes - wanataka wawe wanaongoza kila siku. Ee, tTunataka iwe inazunguka kwa sababu wakenyaWakenya wote ni sawa.

Upande wa interrogation, sijui lakini kuna wakati nilikuwa nikizungumza na mwana sheria rafiki yangu, nikamuliza hiki kifungu cha interrogation kinamanisha nini ukienda kwa Police Station. Utaona kwamba hivi sasa unapoenda kwa Police Station - huyou mwana sheria aliniambia unaposhikwa, ukienda policePolice stationStation unastahili kuhojiwa na ofisa wa polisiPolisi aliyea na cheo ambachyo sio chini ya inspekta. Lakini hivi sasa unaposhikwa ukienda polisiPolisi stationStation utafika pale utakuta hawa waPpolisi wadogo wadogo watakutandika mpaka utaimba kikwenu. Kwa hivyo tunataka hiyo sheria iwekwe katika hali ya kisawasawa hiyo mambo ya kunyanyasa wananchi imalizike. Wananchi wanateseka, tunakaa Kenya kama ambao hatuko Kenya huru. Hiyo itasaidia kwa huuii unyanyasaji wa polisiPolisi kwa wananchi.

Katika uteuzi wa MaD.O.s, MaD.C.s, Ma-Ppermanent Secretaries na MaPCs, hii kitu inatakikana iangaliwe equally. Kwa sababu katika hali ya sasa utakuta ikiwa Mkikuyu ndiye raisRais MaD.O.s, MaDCs, PSs na PCs wengi wao ni Wakikuyu, ikiwa raisRais ni Mkalenjin, wengi wao ni Wwakalenjin, ikiwa ni Mmjaluo wengi wao ni Wajaluo. Sasa Kenya vile tunaendelea tunaelekea tunaonekana hatuna mwelekeo mzuri. Na kuna watu wengine waweza kufanya kazi. Kwa hivyo kwa hii iwe distributed equally katika njia nzuri ili Kenya iwe katika hali nzuri.

Haya, wakati huu utakuta kwamba polisiPolisi mwanaume anakuja kushika mwanamke, na hii inaleta shida sana kwa sababu unakuta hawa polisiPolisi wanaume wanaenda na wanawake wa watu na wasichana wa watu wengine. Tungetaka kwa katibaKatiba kuwe na sheria ambayo polisiPolisi wanaume wanashika wanaume wenzao na polisiPolisi wanawake wanashika wanawake wenzao. Unakuta ya kwamba mtu aliye na ukimwi akaleta ukimwi kwa mtoto wako ambaye alikuwa anajilinda vizuri.

**Com. Wambua:** Bwana Okwirie tafadhali malizia malizia uko na dakika mbili.

**Okwire:** Nina-support sana bwana Robert Kitunga aliyetoka hapa. Haya mambo ya corruption, mpaka yaangaliwe. Kuwe na sheria ya kuangalia mambo ya corruption kabisa. Kwa sababu hii mambo ya corruption hasa sana sana imeingia katika Wwizara ya Llabour. Utaona utafutwa kazi na yule tajiri wako anakwambia, - ukijaribu kusema haki zako, anakwambia “enda popote utakapo. Serikali yote iko mfukoni mwangu”. Na unapoenda enda kwa labour office kweli, ukifika tu wale maofficer wa labour wanakufukuza tu. Kwa sababu kweli tayari wameshatiwa mfukoni na tajiri. Kkwa hivyo kuwe na sheria ya kulinda wafanyi kazi.

Kwa upande wa barabara. Unaona barabara zetu zina taabu na pesa pia ina taabu Kenya. Hao forces, utakuta hawa walioko kwa jeshi na forces zingine, utakuta mwingine ana tumbo hata hawezi kukimbia hata tukiwekwa na yeye tukimbie goli mpaka goli nitamshinda nani mwanajeshi. Kwa sababu wana-relax hawana kitu cha kufanya. Forces wapewe kazi ya kushugulikia

mambo ya barabara. Wasiwe wanakaa tu hivi, na kula na kunywua pombe na bila kufanya practise. Hii itawasaidia for practice wasiwe wanakaa hivi -. Forces wote akina polisiPolisi hawa, ili wapunguze hiyo nguvu yao ya kusumbua wananchi na kupiga wananchi.

Haya, la mwisho;, mtu yeyote ambaye ameshapatikana na kashfa yeyote asiwe anapata cheo cha kuongoza wananchi. Hiyo naungana mkono na wenzangu. Utakuta hata katika serikali yetu kuna wale ambao wanajulikana ni watu wa makshfa, wao ni maprofessors wa corruption na wako katika serikali. Wananchi wanapiga nduru na unaona wako hapo hapo tu. Kila mwaka wako hapo hapo tu. Wengine hata juzi uliona hata wakati wa uchaguzi wa tarehe kumi na nane, watu wanapiga nduru "hapana huyo hatumtaki"- na analetwa hapoa. Kuwe na sheria ambayo inazuia watu kama hawa. Asanteni sana, aliye na swali aniulize.

**Com. Wambua:** Asante sana bwana Okwirie. Kuna swali?. Hakuna swali kwa hivyo jiandikishe upande huiyo. Ulikuwa unataka kuzungumza mama? Nitakupatia nafasi tafadhali.

**Mercy Mwandenje:** Mimi kwa majina naitwa Mercy Mwandenje, I am a teacher by profession na ninasimamia Kenya Society of the physically handicapped, coast region na nina maswala yangu ambayo ningependa kuyazungumza kwa tume Tume hili ili yaweze kutiliwa mkazo katika katibaKatiba ambayo tunataka kuiunda. Sana sana mwenzangu ameyazungumza aliyezungumza, na mimi nami nataka nitilie mkazo maswala ya akina mama walio na ulemavu. Wanawake walio na ulemavu wowote ule, wapewe haki zao za private life na marriage life. Kkwa sababu tunaona kwamba watu wetu walemavu hasa wanawake, hawaolewi kwa sababu kuna interference kutoka kwa wazazi, kutoka kwa friends, kunakuwa na maswali, "kwa nini umempenda mwanamke huyu? Wanawake wazuri walioko dunia hii, ni mwanamke huyu mlemavu ndio unatuletea katika familia yetu? – "Unatuletea kisirani". Kwa hivyo tunaomba katika katibaKatiba, kuwe na huo uhuru wa wanawake. Ikiwa wamekubaliana na mabwana waweze kuolewa bila interference yeyote.

Pili, wanawake walio na ulemavu wapewe haki zao za kurithi mali. Kwa sababu katika mambo hayo yote, mama mlemavu ana shida nyingi na pengine hatapata kuolewa. kwa kutarajia yeye mwenyewe tu kwamba hataki kuolewa mbali na kuwa mabwana hawapatikani. Pia yeye Hawezi kujitegemea mwenyewe na kama hapati bwana wa kumlinda atategemea urithi wa baba au familia yake. Aapewe urithi katika sehemu ile ya baba mzazi. Baba Aajue kwamba, mimi nina mtoto mlemavu na huyo anaweza kuolewa ama kutoolewa. Kwa hivyo ampatie nafasi yake ya urithi.

Tatu, wanawake waliyo na ulemavu wapewe huduma za afya, hasa hapa nimesisitiza reproductive health ili waweze kuangaliwa vizuri kwa sababu wao wenyewe ni walemavu. Na mimi napendekeza kuwa hata tukienda kwa madaktari pia, tuweze kupewa the specialists kwa kuwa hali zetu ni hali ngumu na tusipokuwa waangalifu, tunaweza kuongeza hali hii ya ulemavu kwa huyu mama mlemavu. Kwa hivyo tunauliza kuwa tuweze kulindwa na katibaKatiba, tuweze kupewa medical attention vizuri na hata zaidi, iwe free of charge. Nna kuna watu wetu wengine ambao ni walemavu wana ulemavu zaidi ya moja. Wengine wana kifafa na wako katika medication may be for the whole of their life time. Hawa wapewe hizi madawa free of charge. Kwa hivyo

mapendekezo yangu ni kwamba matibabu kwa akina mama walemavu ama walemavu kwa jumla, iwe free na pia tuweze kuwa attended by specialists kwa sababu ya hali yetu.

Nne, nauliza hii violence against women, akina mama tunapiga kelele sana kwa kupigwa kwa kuwa tunamakosa ama hatuna makosa. Lakini sidhani kama kuna sheria ambayo inamruhusu mtu kumpiga mtu mwingine;, na ikiwa basi violence against women tumeililia sana isiweko, nasisitiza ya kwamba isiweko kabisa katika mama mlemavu. Kwa sababu katika hali hizo za violence inaweza kuongeza disability yake, na ika-worsen the situation. Ikawa pengine alivyokuwa ni bora, kuliko atavyokuwa baadaye. Kwa mfano, ikiwa nitakosana na muume wangu kwa jambo moja au jingine - kwa sababu binadamu si kamili, halafu pengine achukue kisu anitoe jicho, tayari ni mlemavu wa kiwiliwili, halafu anidunge jicho anitoboe niwe pia na ulemavu, - a secondary disability. Hiyo ninasema violence against women especially disabled women, isiweko kabisa. Na mtu atakayepatikana na hiyo violence against disabled women achukuliwe hatua kali. Penalty iwe ile ya hali ya juu kabisa.

Na FGM – female genital mutilation, imezungumzwa sana katika different forums na mimi naisema hapa kwa Ccommission kwamba, hiyo, hasa kwa mama walemavu inaweza hata kumzidisha ulemavu wake. Kwa nini basi ikiwa Mungu ametuumba tulivyoumbwa na kila sehemu ina shughuli zake na umuhimu wake, kwa nini vitu vingine ving'olewe? Kwa sababu gani? Kwa hivyo tunasema hii tulindwe nayo kabisa akina mama. We need every part of our body. Tulindwe kabisa.

Pia nazungumza habari ya harrassment either by polisiPolisi, ama sexual harrassment katika mahali petu pa kazi, pia hasa kwa wanawake walemavu naona pia hapo tumelemewa sana tunasema penalty pia iwe juu. Wale ambao wanawaobaka akina mama na hasa zaidi wanawake walemavu, na hata zaidi nataka kuzungumzia incest hapo. - kKutumiwa vibaya kwa watu wetu walemavu na family members iwe ni baba, iwe ni ndugu, iwe ni mjomba,hiyo penalty iwe miaka kumi na zaidi hata ikizidi sana iwe life imprisonment. Kwa sababu mara nyingi watu wetu walemavu hasa walemavu akili, the mentally disabled children wamekuwa victims of incest., Kkwa hivyo tunaisema kwa sauti kubwa watu wetu walindwe kutokana na incest.

Tumezungumzia habari ya employment kwa muda mrefu ya walemavu kwa ujumla. Mwenzangu amesema 10% za kazi zipewe walemavu na katika ile 10%, akina mama tupewe 5%. Ikiwa 10% ni ya walemavu, basi akina mama walemavu wapewe 5% of that 10%. Iwe nusu kwa nusu. Ikiwa mlemavu hutampa kazi, basi wewe unazidi kumwambia aende barabarani. Right now hapa naona wengi hawako, wako kule mabarabarani. They are making a living - hawana mahali popote pa kwenda, hawajandikwa kazi, wanauza peremende huko barabarani!. Kwa hivyo, sometimes they highly qualify more that their counterparts in different fields lakini hawapewi nafasi kwa sababu mtu anangalia yale ambayo hutaweza kuyafanya zaidi ya yale ambayo uanaweza kuyafanya. Kwa hivyo tunauliza ikiwa ni 10% tumekubaliana hivyo, 5% iwe ni ya akina mama.

Vifpawaa vyetu – mobility Aids, kama Mmikongonjo, wheel- chairs, white- canes, hearing- aids ambazo ni part of our lives, we cannot do without them;, sijui kwa nini vinauzwa.? Magongo haya niliyo nayo ni elfu na.., chuma hiki nilichovaa ni elfu moja na.., viatu vyangu pair moja ni elfu na.. Je! Mtu mlemavu how can they be mobile?. Na kitu kizuri ambacho unaweza kumpatia

mtu mlemavu ni kuwa mobile. Kwa hivyo tunasema, hatukuomba kuwa walemavu. Tuzaliwe Walemavu lakini imekuwa hivi Wengi wetu hatukuzaliwa hivi lakini imetokea kwa sababu fulani na fulani, and we appreciate; tunasema it is a blessing. Kwa hivyo tunaiomba serikali ijue pia sisi, we are Kenyans first and then disabled later. Kwa hivyo watupatie free- of- charge kabisa - tena viwe at a focal point, a central point. Ikiwa ni Mombasa watu wa Mombasa wajue vitu vyetu viko Mmunicipal councilCouncil. Changu kikiharibika niweze kwenda na kuchukua kifaa na niwe mobile. Ikiwa ni wheelchair imeharibika, niende kwa municipal councilCouncil wanipatie hiyo wheelchair na niweze kuendelea na maisha yangu., Kkama mnavyoona leo nimekuja na "raha" mbili; moja imeharibika asubuhi ikanibidi niifanywe 'First Aid'. Na hiyo ya first aid nyingine pia ni mbaya zaidi. Kwa hivyo tunasema, when we talk about things we know because we know where the shoe pinches. Kwa hivyo viwe provided free of charge.

Jambo muhimu sana, ni kuna watu wetu walemavu ambao, they cannot be employed by virtue of their disability. Hawawezi kupewa kazi kwa sababu ya ile hali yao vile walivyo. Kkwa sababu, either hawawezi kutumia mikono yao vizuri, hawawezi kutumia miguu yao vizuri, they are confined to the wheel chairs, japo wamesoma, maana shule ziwazazi wao wamejaribu kuwasomesha, but they cannot be employed. We are asking the Cconstitution iweze kuwatetea wapewe the basic salary of a Kenyan ili waweze kuendelea na maisha. Kwa sababu hawa ni wana Kenya. Ikiwa wataendeleaweza kuachiwa mzigo huyu wazazi, ndio maana tunawaona wengi wao wanaenda kwa streets na wana-beg kwa sababu they need a living.

Finally, - mengine nitaiyaacha katika hii memorandum. Finally, we are talking about maintenance. Maisha ya mtu mlemavu ni magumu kwa sababu kila wakati anahitaji msaada either wa house help, ama wa interpreter kama wewe ni deaf, kama wewe ni blind huwezi kwenda mahali freely without somebody to take you round. Kwa hivyo tunauliza tupate maintenance allowance every month. Kkwa sababu, mimi nikienda shopping wakati huu niamue kwamba nimepata msahara wangu wa elfu zangu kadhaa nataka kuingia supermarket., Bbaada ya kununua vile vitu, mzigo utanishinda, kuubeba siwezi. Itanibidi niite watu wanisaidie na hawawezi kukubebea bure (free of charge) watakwambia 'mama lete shilingi hamsini', kwani mimi si Mkenya? Ile the fact that I am disabled, hainipi ruhusa kama mimi ni extra burden, ya kuwa lazima I must hire somebody, I must hire a taxi, maisha yangu ni magumu sana. Hata tunaelewa wenzetu wanapotravel wenye wheelchairs, wheelchair itakatiwa tikiti, yule mwenye kumsukuma atakatiwa tikiti , yule aliye kwa wheelchair naye atakatiwa tikiti. So wWhat are we saying? Are we telling disabled people not to go anywhere? So, tunauliza allowance. Maintainance allowance ambayo itaweza kutupatia up keep katika mambo yetu yote. Nina mengi, nimeacha kwenye memorandum. Asante sana kwa kunisikiliza na nafikiria ikiwa kuna swali I will respond.

**Com. Wambua:** Asante sana Mercy. Hii maintenance allowance italipwa na nani? Na employers ama ni serikali?

**Mercy:** Infact nilikuwa nimeandika pale, katika census iliyokwisha hatukuhesabiwa kama disabled persons. Kwa hivyo, kwa government yenyewe haijui ina watu wangapi disabled. Kkama ingekuwa imefanya hiyo census vizuri, kukawa na categorisation kwamba watu hawa wetu ni walemavu, then that would be easy; the government would just give us allowances,

we are tax payers.  Sso the government should give those allowances kwa sababu sisi ni Wwana kKenya.

**Com. Wambua:** Kuna swali nyingine hapa.?

**Com. Ayonga:** Mama mwalimu, umeweka uzito mwingi juu ya "violence against women", na ninavyojua, ni kwamba violence ya namna yeyote ni mbaya.  Mbona isingekuwa "violence against anybody"?  Kwa maana nijuavyo, and from experience, nimejua wamama ambao wanakuwa violent against their husbands., Aand these husbands kwa maana ni wanaume, hawataki kusema because katika jamii atakuja fikiriwa ni mtu hafifu sana - anapigwa lakini hawezi na mkewe.  Hawezi kusema kwa maana ni aibu.  Situngeliuliza kwamba, violence ya namna yeyote, kwa mtu yeyote ni kitu kibaya?  Mbona violence against women na isiwe violence against any other person besides the womaen?

**Com. Wambua:** Unataka kujibu – ama ngoja swali la pili.

**Com. Salome:** Ahsante sana Mercy kwa maoni yako.  Tumeyafurahia, hatujapata akina mama wenye ulemavu pahali pengi penye tumeenda kwa hivyo tumefurahia sana hayo maoni.  Mimi nina swali moja.  KatibaKatiba ya sasa, ama sheria ya sasa inakataza incest; yaani uile utumiaji mbaya kwa watoto wowote kutoka kwenye familia.  Sasa, hii ya tatu ungetaka tuiweke kwa kivipi kwa katibaKatiba mpya ndiyo iweze kuwasaidia hasa hawa watoto ambao unasema watoto wa kike wenye akili punguani, ama wapungufu wa kuelewa.  Tungeweka vipi ili waweza kusaidiwa na hii katibaKatiba na waweze kulindwa?

**Mercy:** Nita- respond kwa swali la kwanza la violence against women.  Ni kweli kwamba wako akina baba ambayo they are being violated against by the women.  Llakini ni kwa sababu ya kuwa mama huyu amevumilia kwa muda mrefu mpaka sasa imekuwa amefika kwenye ukuta kabisa.  Ukiona  mwanamke anamkipiga mwanaume, basi ujue amevumilia kwa muda mrefu sana.  Na in most cases, wanaume ndiyo wanaviolate akina mama.  Wanawapiga sana.  Ndiyo nasema kama iko sheria haitekerezwi, na vile tunataka kitekelezwe ni kwamba kuwe na hukumu kali ili akina mama walindwe hasa zaidi wale walemavu walindwe na hicho kifungu.

Na swali la pili katika incest, ni kweli kwamba kunakiko kifungu cha kulinda kutokanahiyo  na incest lakini inatendeka. Inatendeka na mara nyingi inatendeka and may be the mother knows and may be other members of the family know, lakini hawataki kusema kwa sababu ni mambo ya aibu na wanayaweka kama family affairs.  That is why we are saying, ama tunataka kuiweka wazi wazi kwamba iko na inaendelea.  Ndiyo maana ninasema ikiwa tutalindwa na hiyo katibaKatiba, hata mtu wa nje anapojua kuwa kuna kitu kama hicho kinaendelea, awezea kuchukua hiyo hatua ya kutoa hiyo reporti.  Na mimi napendekeza life imprisonment especially for incest.

**Com. Wambua:** Ahsante sana Mercy.  Kwa hivyo utapewa nafasi hapo ujiandikishe.  Tutamwita Samuel Wambugu.

**Samuel Wambugu:** Asante ma-CommissionerCommissioners, asante wananchi. Mimi kwa majina naitwa Samuel Wambugu Githaiga. Niko hapa kutoa maoni yangu ya ukibinafsi…*(Missing part end of Side A)*

**SIDE B**

**…….Joseph:** ...…..... I am Joseph:and justice. Oni langu la kwanza ni kuhusu security. Neno hili security limelewekwa kwa maneno tofauti tofauti. Limefafanuliwa kwa mbinu tofauti tofauti na hasa wana siasa, na wenye uwenezaji wa ile kasumba tulioletewa ya ukabila. Kasumba ya ukabila ilikuja 1992 wakati tulikuwa na hii issue ya multiparty. Hii issue ya section 2A, ndiposa ikaja kuingia ndani ya akili zetu. Ilipoingia ndani ya akili zetu, tumekuwa na aina ya kabila, wengine wakaja wakaletae mambo ya majimbo.

Ningetaka kuzungumzia kuhusu mambo ya majimbo. Majimbo ilipokuja, ilikuja kwa sababu ya insecurity ya uchaguzi. Kabila zingine zilikuwa zinaogopa kabila ndogo. Sasa hivi twasema mambo ya kabila kubwa na kabila ndogo - twazungumzia kuhusu majority na minority. Nikizungumzia kuhusu majority, mimi kama hapa Mombasa nilipo nimezaliwa Maporomokoni huko ya Changamwe mbali na hivyo, niko minority katika Changamwe. Kamau, au Mutuku, au Mutisya, au Koech amezaliwa huko sehemu za mbali huko. Koech amezaliwa Bomet, Mutuku amezaliwa Kitui na yuko hapa Changamwe akiwa minority. Majority walioyokuwa hapa ni Waislam na kabila zingine. Abdala Mwinyi ama mwingine yule, ama Chengo, au Karisa yuko kule Kilifi, yuko kule Kisumu, ama yuko huko sehemu za Nakuru ama yuko Nyeri.

Wale ambao wako huko ndugu zanguni, ni minority katika Nakuru, katika Kisumu, Katika hata North Eastern, - usalama wao umewatia uoga. Kwa hivyo siasa ikawa ni kwamba "sisi minority tunataka uhuru, sisi majority tunataka uhuru". Hiyo imeletea punguani kubwa katika nchi hii. Imeletea matatizo katika nchi hii, imelete mambo mengine ya kushangaza. Kama hapoa mbeleni ndugu zanguni hatujawai kuwa na mambo ya kayabombofire bomb ni hata wengine wakasema kayabombo ni mambo ya mashamba. Haijakuweko hapo mbeleni tukawa tuko na shida ya mambo ya kayabombo.fire bomb (kayabobo). Ndugu zanguni, ile ilioyoko ni insecurity ya kuhusu vile tutakuwa na mwongozo. Vile tutakuwa tumeongozwa. Kwa hivyo mimi ningependekeza, katibaKatiba ilioyoko sasa imezungumzia kuhusu mambo ya violence. Mambo ya wale ambao wanachochea-incitement to violence. Mambo ya uchochezi katika sheria iko.

Lakini pamoja na hivyo, hakuna jambo lolote ambalo limetekelezwa kuhusu wale ambao wanachochea. hHata kuleta maafa ya wananchi. Ningependekeza hasa kwa wale ambao walitoa maoni yao, na katika zile Ccommissions ambazo zimeendelea kuchukuwa maoni na kuona ni kwasababu ya nini hayo yanaendelea. Ni kwa sababu gani watu wamepata matatizo? ni kwa sababu gani wameuana Likoni? wameuana Molo? wameuana na Laikipia? ni kwa sababu gani? yale maoni ambayo yalitolewa na waliohuhusika? katibaKatiba ningetaka iwe wazi na iwe na security ya wenyewe kwamba wenye kuhusika, wachukuliwe hatua. Ikiwa ni kushitakiwa washitakiwe. Ili, wakishitakiwa itakuwa vigumu sana tena kurudia hiyo culture ya violence ambayo inaambatana kila wakati tunakuwa na uchaguzi. Kila wakati tukikaribia uchaguzi tunakuwa na hizo clashes, tunakuwa na hizo

banditry. Kwa hivyo ningesema na ningependa, katibaKatiba itoe mwongozo na isiache wazi kipengele chochote kile ambacho kinaweza kutumika kuhusu mambo ya uchochezi.

Appointment of Ccabinet Mministers;, while the presidentPresident remaintains the power to appoint Ccabinet Mministers after thorough consultations, they must have the foullowing qualifications: -
Have a minimum of a bachelor's degree which is relevant to their ministry; Ffor example an agriculturist should head the Agriculture ministry. A minister for finance should be an economist.

Before the presidentPresident releases the official list it should be taken to Pparliament and be vetted by 2/3 parliamentary majority.
The other one is section three; Wwho should be elected as anthe member of parliamentMP?
He should be a Kenyan citizen.
He should be between 30-80 years old.
He should be above form four education or its equivalent and never a convicted criminal.

Parliament linapaswa lipewe uwezo. MPs should not be allowed to award themselves salaries instead, I'm proposing a Ssalary Ccommission of Kenya to be established so as to review salaries for Ppublic Sservants, MPs, Ccabinet, presidentPresident, Tteacher, Nnurses e.t.c. with regard to the present prevailing economic realities of the day. The sSalary Ccommission of Kenya should be given terms of services and should be the sole decider of all matters concerning salary reviews and increments.

Election of mayorMayors; to strengthen the local government municipality, mayorMayors should be elected directly by the people unlike today wheren they're elected by councilCouncillors. In addition they should have form 4 education or above like the MPs.; Aactually in my opinion they should be treated as MPs.

Education; since every Kenyan is a tax payer, primary education should be free to every Kenyan child and we should have a provision in the constitution Constitution that will cater for semi-arid areas like Moyale, Isiolo and the other remote places of Kenya. Those people should be given a constitution Constitutional provision that will help them to be assisted in that more bursary should be increased in those desert like places. The old 7-4-2-3 system should be revised and be retained. We should do away with 8-4-4 system through thise constitution Constitution reform.

A gender sensitive Cconstitution: An example is chapter 2 of Kenyan constitution Constitution page 6 section 5, 2a. It should say in my opinion; "a person shall qualify to be nominated for election as presidentPresident if he or she is a born citizen of Kenya.

Land ownership; any land that was illegally acquired must be repossessed by the government and be redistributed to genuine squatters. In case of absent landlords who don't make use of their large chunkants of land, though acquired legally, the constitution Constitution should mandate the government to purchase those lands from those absent landlords and redistribute the same.

**Com. Wambua:** Rev. Tafadhali summarize. You can't read the whole memo. We are going to read it. Just highlight.

**Rev. Julius:** Joblessness; the constitution Constitution needs to be strengthened to compel any sitting government to show the number of employment opportunities it has created either through strengthening the private sector, or by expanding its own structures onr yearly basis. The government should be able to account to parliament on every 15th day of May, every year, how it's working to create jobs through clear data that can easily be discussed by MPs.

Voting; constitution Constitution should provide provisions that Kenyan abroad should be able to vote through our embassies abroad. Presidential veto;, the presidentPresidential veto that allows a presidentPresident to reject a motion passed in parliament should be removed..….*continues to side B*

**SIDE B**

***(Continuation)***

**Rev. Julius:** …………. Finally, the new constitution Constitution should be written both in Kiswahili and English and even translated into various vernacular languages. It should never be amended again without consulting the people through a

referendum that will involve parliament, the civic bodies, religious bodies, NGOs and Kenyans in general. May God bless the people of Kenya.

**Com. Wambua:** Thank you very much Reverend. There's a question for you.

**Com. SalomeAudience:** Bwana kasisi sijui kama nilikuelewa vyema. Ulisema kuwa presidentPresident aketi kwa two2 terms minimum na maximum hukutueleza.

**Rev. Julius:** I'm supporting the present constitution Constitution which allows the presidentPresident to be elected after 5 years and he shouldcann'ot exceed 10 years.

**Com. Prof. AyongaAudience:** Reverend, ulisema wale watu wanaochaguliwa wawe hawana makosa, hawajashtakiwa kama criminals before. Llakini nataka pia ufafanue; kuna watu wameshtakiwa kwa ajili ya maoni yao na wakasemwa hao ni watu kisiasa kwamba walikuwa wanajaribu kuharibu mambo lakini wana ideology different kuliko iliyomo serikalini. Je, watu kama hawa waliofungiwa na kutolewa gerezani, unataka kusema mtu aliye na idea tofauti, ideology ambayo ni tofauti, akifungwa hawezi kuchaguliwa baadaye ikiwa watu wameona nuru?

**Rev. Julius:** Hapana. Si maanishi wale wafungwa wa kisiasa;, Kkuna namna mbili za wafungwa wa kisiasa; labda mtu alikuwa anapindua serikali na anaipindua when it's a legally elected government, I think that's a different case. Bbut for political detention of people like Raila who were detained,; those people are not guilty anyway its only that there was a problem during those days. I only mean political convicts not political criminals; people who are real criminals and we have so many in parliament, some have even looted parastatal bodies.

**Com. Prof. AyongaWambua:** Nilitaka tu ufafanue kwamba hii criminality ina mwisho na mwanzo, au ni kila mtu aliyefungwa hawezi kuona parliament.

**Com. Wambua:** Thank you very much Reverend tutamuita Jared Omwandazi, hayuko?. Athman Ali, Timothy Kirigi, Zachariah Odema, Joseph Matata.

**Joseph Matata:** Ahsante sana. Maoni yangu ya kwanza ni kufukuza umaskini. Mtu akiwa ameandikwa kazi, hana ruhusa kuingilia biashara ama kazi nyingine. Kkwa hivyo mtu mmoja kwa kazi moja. Hiyo ndiyo itafukuza umaskini.

Ya pili, hii kuondoa uwezo wa presidentPresident; uwezo huu lazima uweko kwa maana mtu kwa boma hawezi kufukuzwa ama hawezi kuondolewa uwezo wake kwa boma. Kwa hivyo presidentPresident awe na uwezo tofauti na zile zingine. Kile kingine kama ingewezekana ni kuangalia wilaya.; watu walikotoka. Kuna sehemu zilizoendelea kitambo na zingine bado hazijaendelea.

Ili kusawazisha zote, sehemu zilizo nyuma, kuwe na sheria ya kufuatilia ili zisawazishwe na zile sehemu znyingine.

LKingine ni majimbo. Sioni haja ya majimbo;, majimbo si nzuri kwa maana kuna sehemu zisizo na utajiri wowote na zinabebwa na sehemu zingine. Tukiwa na majimbo, sehemu ambazo hazina isio na chochote zitafaidika kutoka wapi?

Kwa elimu; elimu kuna watoto wengi wanaohangaika huko nyumbani na hawa watoto hawana njia ya kujimudu ili waendelee mbele. Kwa hivyo ingewezekana, elimu kwa wale watoto kuanzia std. 1 mpaka std. 8, iwe inaruhusiwa na serikali.

Kingine ni biashara. Kuna watu wenye biashara ndogo ndogo kama vibanda hivi. Kama vile ilivyo, vibanda vilibomolewa; kungekuwa na sheria ya kwamba vile vibanda vikibomolewa, wale watu wanaelekezwa wapi.? Kkwa maana kubomoa na ku-clear kabisa ni kuleta umaskini. Wale watu waliokuwa wanafanya kwa hizvyo vibanda vidogo vidogo wameingia umaskini. Hii ni njia moja inayoapaswa kuangaliwa. Ahsante.

**Com. Wambua:** Ahsante sana Bwana Matata, kuna swali hapa.

**Com. Prof. AyongaAudience:** Bwana Matata, umesema ikiwa mtu ana kazi asiingilie biashara. Mimi nilikuwa nafikiri kuwa kama mtu ana kazi akifungua biashara itasaidia kuajiri watu. Kwa maana investors tulio nao ni watu wamekuwa na kazi na wamepata fedha na ikiwa watafungua kazi za biashara, wananchi wangefaidika kwa kupata kitu cha kufanya. Sasa tukiwakataza watu wasifanye investment ili watu wapate kazi, sasa tutakuwa tumejisaidia vipi? Au ulikuwa unafikiri namna nyingine?

**Bwana Matata:** Hiyo ni kweli. Kama mtu alikuwa amepata pesa kwa kazi halafu ndio awaajiri wengine hilyo ni moja. Lakini unaona mtu anaweza kazi na mwingine hana uwezo, anafanya biashara yake halafu anakuja kuingilia ya yule, anaweka yake. Kwa hivyo ndio nasema, kazi moja kwa mtu mmoja.

**Com. Wambua:** Asante sana Matata. Sasa tutamwita Said Hassan.

**Said Hassan:** Ahsante sana commissionerCommissioner. Mimi naishi mtaa wa Bongo na ninafanya kazi na shirika la KPA (Kenya Ports Authority). Nimekuja kuwakilisha marekebisho kwya katibaKatiba ambayo tunahitaji iwe hivi sasa.

Kwanza kabisa ningependa kusema kwamba, katibaKatiba itakayotungwa hivi sasa ikishakamilishwa na kukubaliwa, isibadilishwe wala isipendelee wala isikeukwe kwa manufaa ya watu fulani; - wakae chini wabadilishe katibaKatiba kwa masilihi yao. Sisi Wwanakenya hatuko tayari. Kama kutatokea mabadilisho yoyote ya katibaKatiba lazima wananchi wajulishwe tena, wafanye referendum ya kubadilisha katibaKatiba.

Jambo ambalo nataka kulizungumzia pia ni kuhusu habari ya kitambulisho. Iwe ni sheria kwa mwananchi kuandikishwa kitambulisho, lakini isiwe ni sheria kubeba kitambulisho. Mwananchi abebe kitambulisho lakini asilazimishwe kwa sababu ya kupotea. Vile vile mwananchi apewe haki ya kuzaliwa bila kusumbuliwa; - birth certificate na passport bila kusumbuliwa.

Mahakama / Jjudiciary; kwa hakika muundo uliopo sasa wa mahakama hautoshelezi mahitaji ya wananchi. Kwanza mahakimu huenda kortini kusikiliza kesi kama wamechelewa sana. Judge anatakikana aingie asubuhi saa mbili lakini anaweza kuja hata saa tano, saa sita anakwenda, saa nane pengine asije kamwe kabisa na kesi zinazorota. Vile vile kesi zisiwekwe kwa muda mrefu; kesi zinakaa sana mahakamani. Mtu anashtakiwa na pengine hana uwezo wa kujikomboa kwa bond anaweza kukaa sShimo la Ttewa miaka mitatu hata miaka minne kesi haijasikilizwa kwa sababu majudge, ule muda wanaofanyia kazi, huwa ni mfupi sana. badala ya kuingia kazini saa mbili, huwa wanakuja saa nne ama saa tano na pengine kesi itasemwa moja tu lakini kuna kesi kama kumi ambazo zataka zisikizwe kwa siku moja ile.

Jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni habari kuhusu serikali za mitaa. Wenzangu wengi wamechangia hapo, wamezungumza kwamba mamayorMamayor na wenye viti vya ubaraza wachaguliwe na wananchi. Hayo mimi nayaiunga mkono na vile vile, maafisi wa baraza la mji (town clerks and treasurers) wapewe mamlaka zaidi kusimamia mabaraza kwa sababu wakiachiwa madiwani pekee yao, hufanya vile wanavyotaka wao.

Kuhusu mfumo wa uchaguzi; mfumo wa sasa hivi wa kura ya siri uendelee kuwa vivyo hivyo na mwenye kura nyingi ndiye atangazwe mshindi. Kuna uhamiaji wa vyama; kwa mfano chama kimekukataa wewe, usiwe nominated kugombea kiti chochote kile, kwa hivyo yeyote atakayetaka kugombea kiti chochote kile aweze kuhama chama kingine; au kama hataki asimame independent bilae kuwa na chama; si lazima mtu kusimama asimame na chama. Hata bila chama anaweza kusimama provided ana support ya wananchi. Nna vile vile wale watu ambao kwamba wamechaguliwa na chama fulani kuwa bungeBungeni, au katika councilCouncil halafu waka-defect, wale wagombeiania wasiruhusiwe kusimama, waruhusiwe wengine.

Kuhusu habari ya bungeBunge; times ambazo Wwabunge wanatumia kule bungeBungeni haziridhishi kwa sababu wanakutana mara tatu kwa wiki na saa zingine bungeBunge yaweza kuahirishwa katikakwa mwiaka karibu miezi mitatu. Utaona kwamba wakati wanaofanyia kazi bungeBungeni ni mdogo sana na hautoshi. Kwa hivyo tunataka times za bungeBunge zifanyiwe marekebisho na vile vile Wwabunge wapewe likizo. Tunajua kwamba mwezi fulani bungeBunge litapumzika mpaka muda fulani. Sio mtu akae tu bungeBungeni anaihairisha bungeBunge halafu pesa na allowances ziyanaliwa bure. Nafikiri mambo ya umilikaji wa ardhi yamezungumzwa na kwa vile wazungumzaji ni wengi, sina haja ya kuyarejea.

Habari kuhusu ajira; napendekeza kwamba 75% ya waajiriwa wawe ni wenyeji wa pale. 25% wawe ni wengine, kwa sababu, imekuja hivi sasa, wenyeji haswa hapa Coast province wamenyanyaswa kiasi cha kwamba hakuna ajira yoyote wanayopata. Yasikitisha kwamba hata hii kazi ya kusoma 'metre' ya taa au maji mpaka zitoke watu kutoka juu. Aau kuchimba mitaro za '

el-nino' ya kuweka nguzo za taa, mpaka watu watoke juu, - hili ni jambo la kusikitisha; Kkwa hivyo tunataka ajira. 75% iwe ni ya watu wa hapa.

Elimu; mfumo wa sasa wa 8-4-4 uondolewe kama alivyozungumza hapa mwenzangu. Huu mfumo haufai kabisa. Ni mfumo ambao umerudisha Kenya nyuma sana kielimu. Tunahitaji mtoto asome mpaka std. 7 kama ilivyokuwa zamani. Akimaliza 7 afanye mtihani aende form 1 mpaka form 4, halafu form 5 mpaka form 6, halafu aende university, - atakuwa amekomaa. Leo inasikitisha, utakuta mtoto mwingine amefika university lakini ukimpa kitu fulani afanye anashindwa. Ningetilia mkazo 'civic education'. - Elimu ya raia iorodheshwe katika katibaKatiba hii. Iwe ni haki. Maana iIkiwa mtoto atajua haki yake kutoka utotoni, akija akiwa mkubwa sio rahisi mtu kama huyo kumnyanyasa. Uwezo wa raisRais upunguzwe. Kkama vile kuchagua Mmawaziri, Mmabalozi na kadhalika. Yeye apewe tu kazi ya kuteuwa halafu hawa wapelekwe bungeBungeni waidhihinrishwe kuwa hawa wanafaa. Kwa hayo, nafikiri nitaachia hapo.

**Com. Wambua:** Asante sana mzee. Kuna swali kwa mzee Said? James Njuguna, Matagaro Ezekiel.

**James Njuguna:** Tume ya Marekebisho ya katibaKatiba, wananchi watukufu, hamjambo? Kuna sheria ambayo ilikuwa inatumika wakati wa ukoloni., Kkwa mfano wakati wa ukoloni ulikuwa unakutana na askari wa kikoloni, wakiwa katika doria wanakushika na kukupiga teke na mambo kama hayo. Katika katibaKatiba hii ikianza kurekebishwa, jambo kama dhuluma ya wananchi iondolewe. Tungetaka pia wakati wa kupiga kura, kwa sababu sisi ni wanademokrasia, sanduku iwe transparent, unaona nje na ndani na wakati wa kuhesabiwa, ihesabiwe papo hapo na mshindi ashinde papa hapo. Isije ikapelekwa Ccomplex hall kama Mombasa,. Ni hayo tu.

**Com. Wambua:** Asante sana mzee Njuguna. Ezekiel Matagaro………….. hayuko. Duncan Mulei, Samson Jera, Mwanakombo Ebrahim Amani, Khasim Musa, Ebrahim Khamis, Consmas yuko? Rukia Athman Kibwana, Ali Juma, Hamed Mohammed, Grace Mbugua. Tuna Muijuma Mohammed, Bakari Ali, Peter Kyema, Gideon Nyamwaya, Lazarus Akungua, Zadi Obayo, Richard Gumbi, Bernard Muyalo, Kalungu Kinga, Shadrack Mutunga, Charles Musau, Festus Chalo, Joseph Omondi.………………………..

**Joseph Omondi:** Mimi ni mkaaji wa hapa Changamwe. Yangu si mengi sana, nitazungumza machache.
Kkwa upande wa uajiri, upande wa wafanyikazi, mimi nashangaa sana migomo imezidi sana Kenya na katika hiyo migomo hakuna siku utasikia wizara ikisema mgomo ni halali. Migomo yote Kenya huwa si halali na utapata kuwa walekama watu wa union wanagepeana zile notice zinazotakikana, lakini unapata hatimaye matakwa yao hayasikilizwi na bado inakuwa ni hivyo hivyo. Kwa hivyo ningetaka ikiwezekana, tume Tume iangalie mambo hayo. Kama itawezekana, kupitishwe kifungo ambacho ikiwa wanaunion wame-exhaust sheria zinazotakikana, wawe wanahalalisha migomo ili wakenyaWakenya waweze kupata manufaa.

Vijana; vijana katika nchi hii wanatumiwa sana wakati wa siasa kama vychombo vycha kufanyia uhuni. Ningependa kuwa licha ya kutumiwa kufanya hooliganism, iwe inawezekana kuwa baada ya election, - na hili ni kuhusu hawa Ma-Councillors na MPs wawe watahifadhi wale vijana kulingana na ile mikataba waliyoandika katika constitution Constitution; maana katika kila chama huwa kuna agenda fulani kwa katika wale vijana. Iwe wataweza kuangaliwa na kuwekwa katika hali nzuri. Naona hayo ni muhimu sana kwa maana tukiangalia siku hizi makazi hakuna, na pia vibanda vimebomolewa, sasa unapata vijana wako hohe hahe, hakuna kitu kabisa ambacho vijana wanaweza kujivunia.

Local authority; kama zitafanywa ziwe katika hali zinazoeleweka zaidi, maendeleo yatapatikana sana katika nchi. Maana unapata Llocal authorities nyingi zimezorota na hakuna plan sawa sawa ambayo inatakikana ifuatwe. Corruption iko zaidi, kila mahali ukienda unapata watu hawaajiriwi, watu wanaajiriwa kwa wingi halafu Llocal authority inashindwa kuwalipa. Sasa unashindwa what's going on. TunNataka kuwe na plan nzuri. Kama powers zipewe mayorMayors, zipewe mayorMayors, kama inapewa Cchief officers, ipewe Cchief officers wawe accountable incase kuna misapproriation of funds, yaani pesa zinatumika vibaya. Yangu ni hayo tu.

**Com. Wambua:** Ahsante sana, maswali? Tutamwita Ali Salim, Jacob Ochola.

**Jacob Ochola:** Mimi ni mkazi wa Changamwe. Mimi kivyangu niliandika 1,600 pages ambazo nikipewa nafasi, I may lecture for over 6 hours - lakini itabidi niseme machache tu. kKwa vile mimi ni Mmkenya na nina haki ya kuongea kama Mmkenya. CommissionerCommissioners ambao tunaona hapa Kenya, nyinyi ndio mliwaajiri na lazima wawafanyie kazi vizuri na lazima muwe na hakika kwamba vzile vitu zote ambazo mtasema si kwamba you're wasting time.

Mimi sijaridhika na vkikao kama hivki maanake huna tuko na KBC Kiswahili service, Baraka FM na hatujasikia matangazo kwamba inatikikana tuje Changamwe hapa, - kumebandikwa tu makaratasi na kuna wanawake na wanaume hawajui kusoma. Ikiwa mngetangaza hivi, wanawake wangekuja wengi; - wanawake ni wengi kushinda wanaume. So this may not be 50% successful.

Affirmative action; hayo mambo ya wanawake kutaka kuwa sawa na wanaume, I think si vizuri sana maanake wanawake wanapaswa kupewa nafasi sawa sawa na wanaume. Hakuna cha mwanamke anasema apewe nafasi sawa sawa na mwanaume na huku anasema anataka achaguliwe 'Pprovincial women's leader'. - h Hakuna kitu kama hicho. Kkwa sababu ukikubali wanawake wapewe affirmative action, watu wataanza kupewa matalaka na Kenya itaharibika.

Provincial administration should be scrapped. Lazima mtoe mambo ya D.O., D.C., P.C. Mimi mwenyewe nilikuwa nafanya harambee, nilijaribu kuwaona hawa watu, it is so hard. It's easy for you to see God than to meet P.C. or D.O - unaweza kumwona Mungu kama hujawaona. Kwa hivyo, munge-retain Cchiefs and Ssub-chiefs kwa maana kwa village, Cchief anaweza kuchapa mtu aliyeiba kuku, huyo mtu akarekebika. Llakini D.O. kama bara kule, watu wa rural hawajui D.O. D.O.

wao ni Cchief na Ssub chief; so scrap D.O, D.C. and P.C.s.

Mayors; they should be directly elected. Hakuna cha mayorMayor ambaye amepate “E’s “kibao”. Hata mwanamke au baba yangu ambaye hajasoma anaweza kupata “E”. “E”. ni kuandika jina lako tu. Kwa hivyo sitaki kusikia mambo ya mayorMayor ama councilCouncillor ambaye hana degree. The minimum qualification should be degree; councilCouncillor, mayorMayor and M.P.

Ningetaka watu wachukue kura wakati wowotekila mara. Hakuna mambo ya siku za kura inapewa kipimo, mnapewa kutoka tarehe 1 hadi tarehe 10. Kura ichukuliwe kila mara. Kkuna mtu mmoja anaitwa Okeyo, aliongea vizuri na singependa kurepeat what he talked about. CommissionerCommissioners huwa niwanaangalia Tt.Vv., Wwengine huwa wanalala kama watu wanatoa mawaidha yao. Jaribuni msilale commissionerCommissioners - if you are serious. Juzi tulisikia katika Tt.Vv, commissionerCommissioner of policePolice alisema kwamba ikiwa kuna torture, corruption au kitu kibaya katika maisha yako, you can report to someone. Tungetaka kujua policePolice akikosea utamreport kwa nani? Utamreport kwa nani ikiwa Cchief amekataa kukusaidia, Iinspector of policePolice amekataa kukusaidia, whom will you report to? Wangetwambia.

ID, vile ilianza, if you go back to the history of education, perharps ndio utaelewa vile ID ilianza. Nningependa ID ipewe kuanzia std. 6, 7 hadi 8. Kila mtoto wa 14, 15, 16 years awe na ID, maanake mambo ya kuwa na ID kama umemaliza shule ni ngumu. Maanake huwezi anza kutafuta ID ya nyanyako - corruption mambo mengi. Nataka kila mtu apate ID at the primary level. Kura mtu apige at 18 years lakini ID before 18 years.

Nomination of Vvice-Cchancellors, Ppermanent Ssecretaries, MDs, Mministers, commissionerCommissioners should be done by a non-specific body. Perharps inatakikana tuwe na Ombudsman katika Kenya. This is my view. We should have Ombudsman and a body that can pick people like PSs and Commissioners. Kila kazi inahitajika ipewe umri fulani. We don’t want to see people who are old and grey-haired wakifanya kazi ambayo watu wengi wangefanya. Kila mtu awe na kazi moja., Bbusiness uanaweza kufungua lakini mambo ya kuwa ushakuzeeka, una pesa nyingi na bado unafanya kazi na wengine hawana.…

**Com. Wambua:** Jacob tafadhali malizia malizia.

**Jacob:** Mombasa inatakiwa iwe na university because it’s a city., Ssi vizuri kwamba kuna Ccity ambayo haina university. Kwa hivyo ingewekwa kwamba to be a city, there should be a university ili watu wanaosoma kwa university wanaofanya parallel degree, wasipate shida. So universities should be in all cities. Watu kama MPs wawe na kipimo cha kufanya kazi. Ikiwa hawafanyi kazi vizuri, wale watu ambao waliwachagua wawe wanaweza kuandika barua ili MPs warudikuje na wakuwe sacked halafu tufanye another kura.

Ya mwisho, KBC is a government body ama Pparastatal na kila mtu ni mwenye KBC. Tunataka mambo ambayo yanatangazwa KBC, isiwe kwamba mtu mmoja anachukua 16 minutes halafu hicho chama chake 7 minutes plus 16 ni 23 minutes ambapo; only two2 minutes inatangazwa mambo ambayo hayana maana kwa wakenyaWakenya,. - Hhalafu tunaenda kwa sports. Ningependa KBC iwe na equal kind of matangazo. Halafu kuna mambo kama National Security Intelligence Service; such bodies are a waste of time. NSHISF should be scraped maanake it's a body within policePolice. Thank you.

**Com. Wambua:** Ulikuwa unauliza ukikosewa na polisiPolisi utareport wapi na baadaye nikasikia ukizungumzia mambo ya ' Ombudsmanubootsman'. Kazi yake ni gani? Maanake kulingana na vile tunaelewa, kazi ya 'Ombudsmanubootsman' ni wale wafanyikazi wa serikali ambao wanafanya kazi kwa njia isiofaa, kazi ya 'ubootsman' Ombudsman' ni kureceive complains kama hizo. Sijui…?

**Jacob Ochola:** Sisemi kwamba watu hawaelewi. We don't have an 'ubootsman' na tuliambiwa kwamba polisiPolisi akikosea unaweza kureport. Mimi nimesema we are supposed to have an 'Ombudsubootsman' lakini mambo ya kureport as per now, tuliambiwa kwa Tt.Vv. last week, kwamba tureport. SAasa of now where can we report to if we are aggrieved?

**Com Wambua:** What we want are proposals to correct the situation as of now.

**Jacob Ochola:** As ofor now, we want a body which can take our views and grievances when we are atleast attacked by policePolicemen and big people.

**Com. Wambua:** Thank you very much. We'vre already noted that. Sasa tutarudi upande wa akina mama. Kuna akina mama wameketi hapa wawili tangu asubuhi Mariam Khalifan…………*continues to tape 4*

**<u>TAPE 4</u>**

**SIDE A**

**Com. Wambua:** Mama akimaliza atafuatiwa na Tatu Mwange.

**Mariam Khalifan:** Ninazungumza maneno yalizungumiziwa, ni kuyatilia mkazo. - kKuhusu hawa watoto mayatima.; Hhii division ya Changamwe ina watoto wengi sana mayatima na wale ambao hawajiwezi na hawana mahali wanaweza kukaua na kuangaliwa. Kwa hivyo mimi nikiwa ni mwenyekiti wa group ya Magongo, naomba serikali itupatie mahali ya kuwakusanya hawa watoto na kuwaweka pamoja, kupata kuangaliwa kwa kula, mavazi na masomo. Naomba serikali iangalie jambo kama hilo la hawa watato wanao tahabirakai. Iwaonee huruma na imani, watupatie mahali tuwajengee. Yangu ni hayo tu.

**Com. Wambua:** Ahsante sana mama,. Yyako yalikuwa mafupi. Tutamwita Tatu naye.

**Tatu Mwange:** MacommissionerCommissioner, wananchi watukufu hamjambo? Mimi ni mzaliwa wa Mombasa kutoka 1939 mpaka wa leo 2002. Nashukuru Mwenyezi Mungu aniongezee umri, niwe na uwezo na nguvu nichanganikane na wenzangu.

Oni la kwanza ni kuhusu mfanyikazi. Mfanyikazi anapofanya kazi ya kampuni, Rreceiver ikiingia kuna kampuni zingine haziwalipi wafanyikazi wale hata kama wamefanya miaka 30 katika kampuni hiylo. Nna katibaKatiba hiyo ni katibaKatiba ya mkoloni. Naomba mkienda kwenye urekebishajimaoni hiyo katibaKatiba iondolewe iwe kwamba mfanyikazi akiajiriwa na akiachishwa kazi kwa receiver ana haki ya kulipwa haki zake.

Maoni ya pili ki kama yafuatavyo. , Kkina mama chipukizi hata wazee, mna haki kugombea haki zenu. Nilisikia Bwana mmoja akisema hamna haki; mna haki. Kugombea haki zenu kKwa cheo chochote kile ambacho kiko karibu nawe ama kiko mbali, kukitafutiea upembo ukiteremshe ukichukue. Naomba viongozi wa tume Tume au wale wa chama hiki cha kuchukua maoni, mchukue jambo hili kama jukumu kwamba mwanamke ana haki ya kupata uwezo wowote popote pale anapoingia.

Nyingine; mayorMayor au councilCouncillor – kiswahili kama sijakosea ni (Mmzee wa Kkijiji;), sioni kutiwe manukato na vitu vingine vya kurembesha ati mpaka awe amefika university ndio aweza kuwa councilCouncillor. Huo ni uwongo. Mtu yeyote ambaye anajiweza na anajisikia mtaa wake anaweza kuhudumu, ana haki ya kusimama kwenye kijiji chake. Ikiwa ni elimu, na Kkingereza, ni vya mzungu. Sisi elimu yetu ni ya Kkiswahili. Narudia lile jambo kwamba watoto wameongezeka mitaani na wanasikitisha, kuanzia Changamwe hadi Mombasa. Mama zao hawajulikani wako wapi na mpaka sasa wasichana wanaendelea kuzaa na kuuwa watoto na kuwaweka kwenye majaa. Mimi ningeomba tume Tume mwende mkaweke katibaKatiba, msichana yeyote atakayeuwa mtoto achukuliwe hatua ya kifo. Na watoto wanaorandaranda, tunaomba serikali itupatie makao ili tuweze kuwasaidia watoto wale wapate elimu ili waweze kujisaidia kesho usoni. Ni hayo tu.

**Com. Wambua :** Mama, kuna swali moja hapa.

**Com. Salome :** Ahsante sana Mama Tatu Mwange kwa maoni yako. Umesema kuwa kina mama wa watoto wakiwaua wauwawe. Nna ningetaka kuuliza, je akina baba - umezungumzia kinaganaga kina mama, tu - je kina baba? Ningetaka kuuliza maoni yako ni gani kwa akina baba kwani wazazi ni wawili wa mtoto.

**Tatu Mwange:** Kulingana na upungufu wa akina baba, asili mia ya wanawake Kenya ni kubwa sana na kila kukikucha, wasichana wanazaliwa. Kkwa hivyo kina baba huwa wale wa kuwachezea wasichana na kutoroka kwenda zao mbio., Mmsichana anabakia hewani hata hajui atafanya nini isipokuwa mzigo ameachia mzazi wake. Kwa hivyo kijana ikiwa atajulikana, kuana haki kijana yule kushtakiwa, kuihudumu mimba ile ya yule msichana na ikiwa atamdanganya msichana ale dawa, kuwana haki wote kwenda jela kwa sababu hiyo ni murder case, wameuwa.

**Com. Wambua:** Ahsante sana Tatu. Naona tumemaliza hiyo list ya akina mama. Nitamwita Richard Kage, Mutuku Mwoki., Ian Mwangi, Jackston Okoth, Mohammed Aman, Benson Atenga.

**Benson Atenga:** Wananchi watukufu nawasalimu Salaam Aleikum? Kwanza, maoni yangu ni kama ifuatavyo; the current constitution Constitution haina preamble na ninaomba macommissioner-Commissioner wakati mnaenda kuandika katibaKatiba, muweke preamble ambayo kwa mfano itakisema kwamba 'sisi wananchi wa Kenya tumeamua katibaKatiba ifuatayo itulinde' amna sheria hizi tuzifuate namna gani.

Uraia;, kulingana na the current Cconstitution, Ccitizenship ni yule mzaliwa wa hiyo nchi kama Kenya, lakini naomba kuwa mtu yeyote ambaye ako Kenya na ana miaka 18, apewe ID., Kkama hakuna ID apewe security social card instead of ID because, I see ID cards don't have any meaning at all.

Employment; I want to request the commissionerCommissioners, when you're going to draft the new Cconstitution, please set a body which will deal with those people who are unemployed. This body will ensure all people and school leavers, will take their names to that body na kazi ikipatikana anapewa kwa sababu unaona kwamba unemployed people ni wengi.

RaisRais; raisRais wa Kenya anatakikana awe mtu aliyesoma kwa sababu watu ambao hawajasoma ndio wameletea shida kwa Iinstitution nyingi za serikali. - mMtu aliyesoma anajua what's management, how to govern people and resources.

Public expenditure; nadhani mtu anayepewa kazi ya pesa inatakikana awe na ujuzi wa pesa. Lakini kulingana na katibaKatiba iliyoko na the system tuliyonayo, mtu yeyote ambaye ni rafiki wa mkubwa fulani, unapewa kazi na unatumia pesa the way heyou likes, because he hasyou have good political will to theyour boss. na Nninaomba mtu atakayekuwa Ccontroller- Aauditor-Ggeneral awe high qualified person for the job. Na mtu asipewe kazi kwa sababu ni relative wa fulani amana ana siasa nzuri na mkubwa kwa mfano kama vilekwa raisRais.

Another thing naomba the new constitution Constitution iweke into consideration, is what we call government of national unity or Coalition government. This I think will save a lot. Sababu si chama ambayo imeshinda uchaguzi itakayo chagua serikali itakuwa all MPs.

Education; there is a saying in Kenya that 'education is for all', hiyo ni uongo. Please set aside funds from the Bbudget for free primary and secondary education. Tunatoa pesa nyingi kwa serikali, kwa nini wanashindwa kulipa.

Another thing is marriage. We have marriage problems because of culture, - utamaduni zilizovurugwa na watu wengi.

Ardhi; unapata mtu mmoja ana acreeka moja na mwingine thelathini. Naomba commissionerCommissioners mkiandika

katibaKatiba, mwandike lazima mtu akuwe na maxzimum acreseka anatakikana apewe. Kama na acreeka kumi kila mtu sawa. Hakuna ambaye anatakikana kuwa na acreeka 500. Ya nini - kwani yeye alizaliwa wapi? Ahsanteni.

**Com. Wambua:** Thank you very much. Kuna swali moja hapa.

**Com. Ayonga:** Umesema kwamba presidentPresident lazima awe amesoma na nina amini kwamba tumekuwa na mapresident pia wamesoma, na hukutuambia ambaye amesoma kiasi gani kwa maana umeendelea kusema mtu ambaye hakusoma, ataharibu mambo. Nna sijui pia elimu hiyo nayo uliyozungumzia ni gani? Unajua tunavyoishi tunazidi kusoma mambo fulani fulani. Kuna wazee hapa Mombasa ambao wanajua mambo tangu nyakati za Sultani mpaka leo ambayo ukimuuliza kijana aliyetoka university hatakwambia mambo hayo. Hao wazee wamesoma Hhistoria yao na iko vichwani mwao na haiyo ni masomo. Sasa hii yako ambayo unasema presidentPresident lazima awe mtu aliyesoma, amesomaje?

**Benson Atenga:** Masomo namaanisha kwamba somebody ambaye ana degree.

**Com. Pastor AyongaAudience:** Unafikiri mtu aliye na degree ndiye amesoma? Wengine wote wasio na madegree hawakusoma? Ahsante.

**Com. Wambua:** Nitasoma majina hapa. Kama unataka kutoa maoni, u-confirm. Kkuna Jared Omwandazi, Pastor Paul Ochieng, M. A. Sheikh Atibu.

**Mzee Manicipaa Ngonyo:** Ahsante sana Bwana CommissionerCommissioner na ndugu zangu, wake kwa waume, salamu aleikum?. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi. Nilizaliwa 1942 lakini maoni yangu ni kuwa ugonjwa ulioko hapa ni ugonjwa wa ardhi na makao. Nchi zilizokuwa zimekaliwa na Wwabeberu, walipokimbia zilichukuliwa na serikali na kurudishwa hapa. Ziliporudishwa wale wazee waliokuwa wakifanya kazi kule hawakulipwa chochote, wakabaki pale shambani, wakafa pale pale mpaka sisi tukazaliwa pale. Shida ni kwamba, kutoka zamani iko hiyo nafasi ya kila mtu kupata haki yake lakini ilikuwa hakuna mtu wakujitokeza kusema sisi tumezaliwa hapa. Kwa hivyo utakuta ikiwa ni Nairobi, ama wapi, wale waliambiwa wajiandikishe citizen, waliokataa walikwenda zao, nyumba zilichukuliwa. Kwa hivyo yale mashamba huchukuliwa na kampuni, wale wananchi wanahangaika hawana mahali pa kukaa. Masikitiko yanaendelea mpaka dakika hii, - tutakwenda wapi? Ikiwa sisi tu wanahuru tutakwenda wapi? Kwa hivyo kitu cha kwanza ichukuliwe hii habari ya mtu pale alipo, hii commissionerCommissioner yetu ambaye itaingia kwako ichukulie kwamba ni neno la katibaKatiba ya mtu ambaye hana makao apewe makao kisha apatiwe title deed ajihudumu kama mwananchi wa kawaida.

Pili, kumetajwa mambo ya policePolice. PolisiPolisi ni kweli ni kazi yake anaweza kukushika wakati wowote lakini pia liingizwe kwa katibaKatiba, ikiwa polisiPolisi atawashika, hatujui ni mahali gani pamewekwa kibao. Ukifika unaambiwa keti hapo, ukiketi unalazimishwa kuwa unavuta bangi au unakunywa tembo na mimi sinywi tembo. Judge akishaambiwa huyu mzee

ameshikwa na kitu fulani anakubali, mimi nakwenda kufungiwa kule, kazi yangu inaharibika. Kwa hivyo, katibaKatiba bwana Ccommisioner, itiwe oni kwamba polisiPolisi wakisumbua wananchi wawashike, wawe na thibitisho halisi. Wasishike wananchi vivi hivi.

Ya tatu ni vile unasikia majimbo; tunakitaka kiingizwe kwa katibaKatiba kwa sababu watoto na mabibi zetu wanaweza kuandikwa hapa. Sio kwamba watoto wetu wakose kazi, waandikwe watu zaidi kutoka juu. Hiyo katibaKatiba iangalie haki ya wenyeji; wale wakaaji wa hapa. Nimetoa maoni ya kupendekeza katibaKatiba kutoka Miritini ward, Mpirani KCC, huiko ndiko nimezaliwa. Tunaomba pia baadala ya kupatiwa hayo makao, tuletewe na maofisa wa Aagriculture . watTuonyeshwe kulima.

**Com. Wambua:** Tumwite Mwariga Moka Nyange.

**Mwariga M.:** Nimekuja kuzungumzia maneno kwa tume Tume hili na nashukuru macommissioner-Commissioners mliokuja kusikiliza maoni yetu. Mimi ni mzaliwa wa Pwani, mimi ni Mmtaita. Shida tuliyonayo Pwani ni kuhusu mambo ya reli. Reli hii imeanzia Mombasa mpaka Taita ikaendelea huko mbele kwengineko. Llakini hapa, hapa imegawanya Kilifi na Kwale. Utaona kama 10 metres ya nyumba iko Kwale, kati kati ni reli, 10 metres nyumba nyingine pia iko Kilifi na sisi tunaonana, na utaona tu kwamba watu hawa wamewekewa vikwazo na reli. Akikanyanga reli tu, anashikwa. Akipelekwa mahakamani anahukumiwa kama mtu aliyeuwa mtuna; miaka miwili. Hivi ninavyosema, kuna wenzangu tulishikwa juzi. Tulitozwa fine Shs. 20,000 kukanyaga tu! Nna aliyekosa alifungwa 2 years. Hivi ninavyosema wanatumikia vifungo. Mimi nafikiri kwamba uhuru huu ni wetu na shida hizi ni zetu. Tusipozitatua sisi hakuna atakayetusaidia. Tunaomba tume Tume hili lipelekwe maombi yetu kwamba “kanyaga” (reli) iondolewe, watoe amri nyingine. Lakini kukanyaga kwenye reli, iondolewe kwa maana hiyo reli iko kati yetu sisi.

Mnyama akiruka huku na kukanyanga shamba zetu anakanyanga, yeye, hana makosa;. Lakini sisi tukikanyanga kwa huyu mnyama, tuna makosa. Utaona hapa ninapoelezea ni kwamba unatoka hapa sasa ukifika karibu na Voi, unaona tu wanyama wako upande huu na sisi tuko upande huu. Lakini mnyama huyu akikanyanga kwetu sisi hakuna makosa. Lakini mwanadamu akikanyanga kwa mnyama anapigwa risasi. Hiyo ni haki? Sasa mwanadamu ndiye utu au utu ni mnyama? Commission hii ituangalilie tuwekwe kwenye katibaKatiba maanake mambo haya ya katibaKatiba ndiyo yatatusaidia zaidi.

Sisi watu wa Pwani tuna taabu, ukiangalia skuli, tuko na skuli ya vipofu hapa. Skuli ya vipofu iko hapa Likoni pekee yake. Haina sekondari na ukitazama Kenya nzima, utakuta kule Thika ndiyo utapata ile sekondari. Ssasa wale watoto wetu walioko hapa wanasoma wakipita wanakwenda Thika. Ukitazama kutoka hapa hadi Thika ni pesa ngapi? Pesa nyingi sana. Tungesema serikali ituonee huruma itupatie sekondari nyingine hapa ya vipofu maanake kumsomesha kipofu ni kujikazakazi moyo. maanake hujui atakuja kukusaidia lini. Ni mwana wa Mungu huyo. Kwa hivyo tunaomba skuli hizo tupatiwe.

Sisi twaonewa sana na watu wa kutoka huko juu. Wenzetu wanatulalia sana. Unaona tunawakaribisha watu maana tunapenda watu sana halafu wanaanza kututawala. Tazama Taveta. Utakuta tu mbungeMbunge ni Mkamba. Mtu huyu anajua mila za Wwataita? Hajui. Sasa tuliukataa ukoloni tunarudiwa na ukoloni mwingine. Maskini hatuna na la kufanya maanake atamsaidia Mmkamba latuu hatanisaidia mimi Mtaita na anajua wazi kwamba mimi sikumpigia kura. Kwa hivyo ikiwa mtu atajiandikisha mpiga kura ni mpaka awe wa pale pale. Nndio hivyo sisi, tume Tume, wla Mombasa tunataka hivyo.

**Com. Wambua:** Ahsante sana. Tumuite Paul Anyando

**Paul Anyando:** Hamjambo wananchi wote?. Nimezaliwa KuBbara. Mimi kwa maoni yangu ni kuwa Katiba ni Katiba ile ambayo inaangalia rRaia. – na raia ni sisi. Pia lingine ni juu ya uchumi wetu. Uchumi uko chini sana na watu wengine hawana kazi. Kenya ni nchi ya watu million nyingi lakini utapata ni watu kama million tano tu ndio wako na kazi. Hii inakuwa shida kwa walemavu ambao hawana kazi. Mimi ningeomba Serikali ifungue makampuni nyingi ili watu wapate kazi ili Kenya iendelee mbele. Sina mengi yangu ni hayo. Ushuru uko juu sana na watu wengi hawana kazi. Tuko watu wengi sana na ni milioni tano tu wanaofanya kazi. Na sasa walemavu watafanya nini kama hawana kazi? Naomba serikali ifungue kampuni zingine ili watu wengi waweze kupata kazi ili tuendeleze Kenya. Kenya inarudi nyuma kwa sababu ya ukosefu wa kazi. Naomba hayo kwa leo hii.

**Com. Wambua:** Mainga Nzili.

**Mainga Nzili:** Kwa jina naita Maiga Nzili. Maoni yangu kwa serikali hii tuliyonayo, ni kuwa iko baridi sana maana hatujui kama tuko kwa serikali. Ukienda dukani, unakuta kila kitu bei mbali mbali. Moja hiyo.

Ya pili, watawala wetu hawajui kwamba wanatutawala sisi. Wakikupata hivi hivi wanakuweka ndani na wanakuandikia makosa yasiyo yako. Sisi tunataka serikali inayofaa, itakayoangalia maneno yote ya raia na shida zote za raia. Sina mengi ya kusema ni hayo tu.

**Com. Wambua:** Ahsante sana Mzee Nzili. Tumwite Khamis Juma.- half a minute.

**Khamis Juma:** Kwa jina ni Khamis Juma Maguzo kutoka Kipe Voi. Natilia mkazo sana swala la mayorMayor. Kwamba achaguliwe na raia. Kutakuwa hakuna ulaghai wowote utakaopitia kwa mfano njia ya macouncillor na kuhongwa ili mradi warudishe mtu wanaomtaka. Lazima hili lifuatiliziwe kuonekane kwamba raia wamepewa uwezo wa kuchagua mayorMayor.

Ya pili ni kuhusu Kadhi mkuu (Chief Kadhi). Ningeomba tume Tume hili limpe mamlaka Chief Kadhi wa Islam kama mamlaka ya Attorney- Ggeneral kuwa maslahi ya Uwaislamu kulingana na kesi zao kwa sababu kuna kesi kwa mfano kama ndoa. Unakuta mara nyingi tunakosea desturi na sheria za dini. Unakuta mtu anaenda kufanya ndoa na mtu ambaye niachukuwa

Mmuislamu kwa DC. Ingekuwa vizuri kila dini ipewe heshima yake kulingana na utaratibu wake. Kwa hivyo Chief Kkadhi apewe nguvu atumie sheria yake kulingana na Kkitabu alichopewa dhidi ya Wwaislamu. Ahsante.

**Com. Wambua:** Tutamwita Mzee Mwisumidali

**Mwisumidali:** Nawakilisha Wamini Foundation. Nataka kuzungumza kuhusu kifungu 69 cha katibaKatiba juu ya ucChief Kkadhi ambayo hii iliwekwa kufuatia mkataba uliofanywa Lancaster House 1962. Ningetaka huu waadhifa wa Cchief Kkadhi ubakie katika katibaKatiba na upanuliwe.

Raia; kifungu 87 cha katibaKatiba yetu yasema awe ni wa race gani mtu aweza kuwa raia wa Kenya. Llakini ukiangalia kifungu cha 97, imesema kuwa ikiwa mtu ana uraia mwingine, mpaka a-renounce. Mimi nafikiria wakenyaWakenya waruhusiwe wawe na dual citizenship. Ikiwa mtu ni Mkenya halafu ameenda Uuarabuni au nchi nyingine; amechukuwa uraia kule, aruhusiwe kuwa raia kule na hapa kwao vile vile.

Judicial Service Commission; Kifungu cha 68 cha katibaKatiba ya sasa chasema kutakuwa na JSC ambayo mwenyekiti wake ni Cchief Jjustice na Aattorney Ggeneral ni member. na Majudge wawili watakaochaguliwa na raisRais pamoja na Cchairman wa Public Sservice Ccommission. Nafikiria tukifuatana na kifungu cha 66 juu ya uadhifa wa Cchief Kkadhi, nafikiria kuwa Cchief Kkadhi pia angekuwa ni member wa Judicial Service Commission, kwa sababu Mmakadhi wote wanaandikwa na hili tume Tume ya JSC. Kkwa hivyo itakuwa ni ukosefu au upungufu mkubwa kama makadhi wa Kenya watachaguliwa na JSC na Cchief Kkadhi hayuko katika lile tume. Naomba katika hili tume Tume yna JSC, they include the Cchief Kkadhi as a member. Nafikiri nimemaliza.

**Com. Wambua:** Ahsante sana mzee. Kabla hatujawaita akina mama, tumwite Musa Rasi.

**Musa Hassan Rasi:** Kwa majina naitwa Musa Hasan Rasi. CommissionerCommissioners, mabibi na mabwana hamjambo? Kile ningetaka kuchangia katika katibaKatiba hili mpya ni kuhusu maisha ya wale walioko magereznyumbani. Ningependa katibaKatiba iwapatie walioko magerezani nafasi angalau kwa mwezi mara moja wapate kujamiana kama mtu atakuwako na marriage certificate. Angalau bibi akienda kumtembelea bwanake aliyefungwa, waweze kujamiana na ikiwa ni bibi, iwe ni hivyo. Hii itapunguza kule kulawitiana, - wanaume kwa wanaume wanalawitiana sana. Hii itapunguza Uukimwi, na pia ningeomba katibaKatiba mpya ijayo ishughulikie swala hili. Pia jambo lingine, angalau wale wafungwa waishi maisha mazuri, wapewe Tt.Vv. ni piaama wavae suruali ndefu. Wakija huku nje, huwa wako katika hali mbaya sana. ningependa katibaKatiba mpya iangalie mambo hayo. Ni hayo tu. (clapping)

**Com. Wambua:** Ahsante sana. Tumwite Bi. Mvuua Javar.n

**Mvuua Javan:** Jina langu naitwa bi Mvuua Javarn. Mimi ni mama katika Changamwe Division Leader. Jambo la kwanza ni kuhusu bibi na bwana. Bibi atamwoa bwana wakiwa wote wawili hohe hahe, watakaa pamoja wachume, alafuhalafu bwana atamtoroka bibi amwache na watoto. Naomba bwana yeyote atakayemuoa bibi ambaye ni bikira, wachume pamoja, asimtupe yule bibi kwa sababu akifanya hivyo atakuwa ashamharibia yule bibi maisha yake. Hataweza kuwa bikira kama alivyokuwa mwanzo. Bwana atamwacha bibi aende akatafute mwingine mchanga halafu mali yote waliyochuma, yule mama hatapata. Naomba katibaKatiba ikiwa mama na baba wameonlewa ile mali akimfukuza bibi, ili apewe haki yake na watoto.

Eda; naomba, Eeda ipitishwe kwamba mama wa Kkiislamu akifiwa na mumewe, akiwa yuko nyumbani, atakuwa ana matatizo - na kama mama anafanya kazi 'hususwan'. Ikiwa mama amefiliwa na bwanake, mama hana mahali atakapotoa chochote isipokuwa ofisi anayofanya kazi bwanake, imhudumie yule mama kwa miezi minne na siku kumi mpaka atakapomaliza eda akiangalia mambo mengine baadaye.

Kuhusu Passport na vitambulisho; Bbabua zetu walikuja hapa Kenya kufanya biashara, wengine walikuja kujenga reli, leo mtu akipataka passport au kitambulisho, anaambiwa atoe kitambulisho cha babu wa babu yake. Atakitoa wapi? Ikiwa baba yake ni mzaliwa wa hapa na mamake ni mzaliwa wa hapa?. Mtu yeyote ambaye ni Mmuislamu, ana jina la Kkiislamu huwa anapata shida kupata kitambulisho au passport. Aambiwa aende Nairobi. Tunaambiwa Mombasa ni city, aende Nairobi kutafuta nini? Naomba hii iwekwe kwenye katibaKatiba kuwa mtu yeyote aliyezaliwa Kenya ni Mmkenya. Babake amezaliwa hapa. Haina haja kuambiwa aende kutafuta kitambulisho cha babu na babu na babu. Atakipata wapi? Na wazee wetu walikuja hapa kufanya biashara na kujenga reli na wakaoa wananchi wa hapa; watarudi wapi? Kwa hivyo ili liangaliwe katika Katiba.

La mwisho ni kuhusu MPs; MPps wanakwenda kwenye bungeBunge, wanapanga mishahara mikubwa mikubwa na kura wamepewa na sisi wananchi. Isitoshe mishahara iyale wanatumia kwa miaka mitano. Sasa kuna scheme imeletwa ya pension kwa Wwabunge. Sisi wananchi ndio tumewapeleka hao Bunge. Halafu yeye anakaa huko miaka mitano. Akitoka hapo akishinda akishindwa, anajua ana pension atakula Atakula hii pension mpaka kufa kwake. Je, yule maskini aliyempa yule mbungeMbunge kura atakula wapi? Naomba hiyo pension isiwekopasiwe na ile pension ya wabunge. Ni hayo tu.

**Com. Wambua:** Tutamwita Serafin Charo.

**Serafin Charo:** Nafanya kazi na shirika la YWCA. Ningependa tu kutia mkazo katika preamble. Constitution Constitution yetu iwe na preamble na katika hiyo preamble ieleze kuwa Katiba preamble ni ya Mmwanakenya na pia tuweze kumtambua Mwenyezi Mungu kuwa ndiye anayewezesha nchi kuwa na maendeleo.

Pili, katibaKatiba yetu iwe na sehemu ya watoto. Watoto waruhusiwe kuwa na majina na nchi, na mtoto awe Mmkenya kama amezaliwa na mwanamke Mmkenya au mwanamume Mmkenya. Pia ni vizuri kuwa mtoto yeyote awe anatunzwa na mama na baba aliyemzaa. Hii itazuia watu kuzaa hapa na pale - ili waweze kuchukua jukumu lya kulea watoto ambao watawaweza.

Wote wachukuwe majukumu mama na baba.

Pia tungependa kuwa sehemu ya akina mama ya affirmative action,; si kusema kuwa ni wavivu au wa chini lakini tunataka kuwainua wafikie lile lengo kuwa kila mama aweze kupewa nafasi ……………..

*(Side A finishes)*

**SIDE B – *(Continuation)***

Hii hali ya kumiliki pia; watu waambiwe kama unaweza kuwa na nyumba kama kumi au ekari 50, ili wale ambao ni wagonjwa wa ku-grap, wa-grab mpaka hapo ndio wanawacha mpaka walio na tabia ya kugrab, wanagrab mpaka constitution Constitution imewakubali kugrab mpaka hapo wanawacha wengine nao wanawezea kuendelea. Kwa hayo machache nNashukuru.

**Com. Wambua:** Ahsante sana kwa hayo machache. Tutamwita Rehema. Rehema hayuko? Nafasi yake tuipatiempe Mzee Omar Matano.

**Omar Matano:** Jina langu ni Omar Matano ni mkaazi wa Bomu Magongo.

Kuna Vitu viwili ambayo nataka kuzungumzia: Ya kwanzmba ni administration ya nchi.. Ya pili ni management ya hiilo nchi yetu. Mpangilio ulioyokoi hivi sasa si mpangilio mzuri. Nchi yetu imegawanywa kimajimbo. North-eastern, Coast, Eastern, Central. - mMpangilio huu ni mbaya sana. Ndio kitu ambacho kinaleta huu ukabila. Napendelea kuwe na constituencies, Kenya nzima igawanywe into contituencies ambayo haita-take care about this tribe, religion or anything. Hivyo ile constituency zitakuwa na watu wanaozisimamia, na wao yeye ndioye watakuwa MPs. Constituency moja yaweza kugawanywa into 4 wards, kila moja iwe na Cchief, ambaye sasa anaitwa councilCouncillor. Cconstituency kama tatu, nne au tano, ziunganishwe ziitwe councilCouncil. Hiyo councilCouncil ndiyo itakayoweza kukaa pamoja. Members wake watakuwa nani? Atakuwa ni huyo mbungeMbunge na hao Mmachifu. Hao ndio watakaoendesha mambo ya sehemu hiyo.

Kila Mmwanakenya itakuwa a-belong to a certain constituency. Wewe mwenyewe useme unataka constituency gani. Utakuwa pale ndiko kwenu. uUkichagua constituency yako, tuseme ni ya sehemu fulani basi hapo ndipo penu sasa; ukiwa Mmkamba, Mmkikuyu, Mmtaita e.t.c. itakuwa rahisi kwa serikali kuhudumia watu wa constituency moja. Hapo ndipo utapigia kura. Siku ya watu kuandikisha kura, wewe itabidi uchukue yako katika hiyo constituency uliochagua mwenyewe;. Sasa tut Twampa kila Mmkenya kwake. - hHuna ruhusa siku ya kura ikifika, kuchukua ID card yako kutoka hapa, wewe ni Mkamba na kwenda Uukambani kujiandikisha kura, wewe .ni Mkamba utoke Ukambani ati uje hapa ujiandikishe kura; aah! ID yako inaonyesha wazi kwenu kule ulichagua kupiga kura – kule Ukambani.

Pia ikiwa hapa ndipo pako, ukifariki hakuna kupelekwa mahali pengine kuzikwa utazikwa papa hapa. Hiyo ndio upande wa administration ambayo mimi naonelea ndio itakayapoondoza hii chuki za ukabila.

